





**Askari** polisi wanaodaiwa kumuua mkulima wakamatwa

UKURASA 5



**POSHY QUEEN KUACHIKA NI AJABU?**

UKURASA 20


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 5, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580967

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Vifo vya watu 90 vyashtua

• **Ni** wanaodaiwa kuuawa na askari hifadhini, kuliwa na wanyama... *Endelea ukurasa 2*



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson



Philipo Mulugo



Mwita Waitara

## Mikoa hatari kwa kelele yatajwa

UKURASA 2



## ‘Moshi mweupe’ gesi asilia, Samia aita wazabuni wazawa

UKURASA 3


**MICHEZO** | **YANGA WAMZUIA MAYELE** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6




Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Benson Kigaila (kushoto), akikabidhi kadi ya uanachama wa chama hicho, kwa aliyekuwa Mwanachama wa ACT-Wazalendo, Mariam Hamadi, wakati wa Kongamano la Vuguvugu la Katiba Mpya, jijini Tanga jana. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Vifo vya watu 90 vyashtua

**Na Romana Mallya**

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, amempa siku tatu mpaka Jumanne ijayo Mbunge wa Tarime Vijijini, Mwita Waitara, kuwasilisha ofisini kwake ushahidi dhidi ya taarifa za mauaji ya watu 10 aliodai bungeni jijini hapa juzi kwamba wameuawa jimboni kwake kutokana na migogoro ya ardhi.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa agizo hilo juzi jioni bungeni wakati mbunge huyo akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Waitara alisema kuwa kule Tarime Vijijini ambako ni jimboni kwake, Rais Samia Suluhu Hassan alikwenda na kukuta tume iliyoundwa na mtangulizi wake, Rais John Magufuli na akafanya uamuzi wa kupeleka timu ya mawaziri wanane kutatua kero zilizoko.

"Ninasikitika tangu nimezungumza hapa wakati wa hotuba ya Waziri Mkuu, wizara hatujawasiliana wala wahusika na kule kwenye mgogoro hawajafika, watu wangu wanalalamika. Vilevile, kuna vijiji 975 ambavyo vinahusika katika maeneo mbalimbali kwenye migogoro ya ardhi.

"Jambo kubwa ambalo wizara lazima ilibebe na ilifanye kama Rais amesimamia The Royal Tour na watalii wanakuja, ndege zinaongezeka, lazima tutatue migogoro ya wananchi, itakuwa haina maana kama tunapata faida ya watalii kuongezeka halafu migogoro ipo katika maeneo yetu, inatia doa," alilalamika.

Mbunge huyo alimwambia waziri mwenye dhamana na maliasili na utalii kuwa ana kazi kubwa na kwamba angechangia kwa tofauti kama mtangulizi wake, Dk. Damas Ndumbaro, angekuwapo wizarani hapo.

"Nilimwambia mara kadhaa tangu mwaka 2020 aende Tarime, Nyanungu, Ngoronya, Kwihancha, hawajawahi kwenda kusikiliza wananchi wangu na wanalalamika," alisema.

Waitara alisema Wilaya ya Tarime ina kata tatu ambazo zina mgogoro na Hifadhi ya Taifa Serengeti, hasa vijiji saba ambavyo alivitaja bungeni.

"Mgogoro huu unagusa watu wa Bunda, Serengeti, Butiama mpaka Rorya, ukienda Kijiji cha Masanga, Kemosabi, Kegonga, Nyandage Katonga, Nyabirungu kote kuna mgogoro mkubwa," alibainisha.

Alisema yapo mambo ambayo yanafanyika Tarime yanatesa watu na kuna maeneo wananchi wameuawa.

"Mtu analishwa mizoga, wengine wanalishwa pilipili mpaka wamekuwa vipofu, pia wanachoma nyumba za watu, wanaharibu mazao ya watu. Hili jambo siyo zuri.

"Ukienda Kata ya Korong'a kuna watu 10 wameuawa (akawataja majina yao), miili mingine ilipotea kupoteza ushahidi.

"Tume zimeundwa nyingi, hao ni waliokufa, wapo waliopigwa risasi walikuwa saba (akawataja majina yao), wamepigwa risasi, wapo walemavu. Bahati mbaya katika eneo hili unaunda tume lakini gari lenyewe tunalalamikia watu wa Serengeti wanatoa gari, posho wanatoa hoteli, wanaandaa chakula, ripoti zote Mheshimiwa Spika hazijawahi kutoka.

"Nikisema haya mambo utasema ninatunga, lakini Mheshimiwa Waziri baada ya Bunge hili, aende Jimbo la Tarime Vijijni aone haya mambo ni ya uongo au ni kweli?

"Hao ninaowazungumzia wapo na nimeindikia barua wizara hii kwamba 'nendeni mkawasikilize'," Waitara aliwasilisha kilio cha wananchi bungeni.

Baada ya kusema hivyo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, alisimama na kuomba aweke kumbukumbu sawa.

"Ninampa taarifa anaposema mawaziri wanane hawajafika, katika mikoa ambayo imetembelewa na ile timu ya mawaziri wanane mkoa wake ni mmojawapo.

"Tumekwenda mara mbili, timu ya kwanza ilikwenda ikiongozwa na Mheshimiwa (William) Lukuvi, walikwenda mpaka vijijini, ile ya pili tumekwenda na tumeongea na uongozi wa mkoa na maelezo yote yametoka.

"Unaposema hawajakwenda, aweke kumbukumbu vizuri kwa sababu tunaweza kupotosha kwa kitu ambacho siyo sahihi sana," waziri huyo alitoa angalizo.

Baada ya taarifa hiyo, Mbunge Waitara alisema hataki kubishana na waziri, lakini anachoweza kusema walikwenda wakaishia mjini Musoma, hawakwenda katika maeneo aliyoyataja awali.

Mbunge huyo alisema mgogoro uliopo ni kwamba bikoni ambazo zinatangazwa za mwaka 1968 na wananchi wanabishania siyo kweli.

"Kuhancha walivyokwenda wataalamu wakakutana na viongozi wa wananchi, wale wazee mgogoro umekwisha.

"Koronga, Nyamungu bikoni wanasema ni za kwao, ni eneo la hifadhi, watu wamezaliwa pale miaka 1980 wameishi, ukienda na kukaa nao watakwambia bahati nzuri eneo hili watu waliozaliwa pale wameongoza udiwani miaka 20, ninaomba Mheshimiwa Waziri na wenzake watume watu wakaongee na wale wazee au niweke hapa uwasikilize?" alihoji.

Waitara pia alisema ipo mifugo ambayo imekamatwa, akitolea mfano mifugo iliyokamatwa Nyangage, japo hakutaja tarehe ya kushikiliwa kwa mifugo hiyo.

Baada ya maelezo hayo, Spika alimwita Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, George Simbachawene, ambaye alisema mbunge huyo ni kiongozi wa miaka mingi.

"Uwakilishi wetu sisi wabunge siyo kusema tu ndani ya Bunge, ipo mifumo mbalimbali ambayo tunakutana Bunge na serikali, kulileta hapa jambo zito kwa maelezo ya namna ile mauaji, risasi hakuna kinachofanyika ni tuhuma nzito ambazo kweli zinahitaji tafakuri," Simbachawene aliweka angalizo.

Spika Tulia alisema: "Huwezi kusema watu wameuawa kama amefariki, wanaofariki wako wengi, watu wanaumwa malaria na nini, ukisema mtu ameuawa maana yake kuna ushahidi unaoashiria kuna mtu kamuua mwingine," alisitiza.

Alisema jambo hilo ni zito na wapo kwenye wizara ambayo wameleta hoja ili wapitishiwe.

"Ushahidi ulionao niletee mimi ili niiagize serikali kuhusu jambo hili kwa sababu tuhuma hizi ulizozitoa ni nzito," Spika Tulia aliagiza huku Waitara akijibu kwa kuahidi kutekeleza alichoagizwa na kiongozi huyo wa Bunge.

Spika alimweleza mbunge huyo kuwa amempa muda mpaka Jumanne awe amepata ushahidi wa yote aliyosema.

**MULUGO NAYE...**

Uamuzi kama huo pia ulitolewa na Spika Tulia dhidi ya Mbunge wa Songwe, Philip Mulugo, aliyedai watu 80 wameuawa kwa kuliwa na wanyama na wengine kujeruhiwa na kubaki na ulemavu wa kudumu.

Mulugo alisema amekusanya ushahidi wa kutosha kutoka katika halmashauri yake pamoja na wananchi.

# Mikoa hatari zaidi kwa kelele hii hapa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BARAZA la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (NEMC) limetaja mikoa mitatu inayoongoza kwa malalamiko ya kelele kuwa ni Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma.

Vilevile, limebainisha kuwa nyumba za ibada na maeneo ya starehe yanaoongoza kwa kulalamikiwa kuwa na kelele.

Akizungumza jana kwenye warsha ya Maofisa Mazingira wa Mikoa na Wilaya, Meneja wa Uzingatiaji wa Sheria na Ufuatiliaji kutoka NEMC, Ndimbumi Mboneke, alisema:

"Siku za hivi karibuni kumekuwapo na shida sana ya kelele kutoka kwenye maeneo mbalimbali nyumba za ibada, kumbi za starehe, baa na viwanda mbalimbali, hii inatokana na kukua kwa teknolojia, kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kibinadamu."

Meneja huyo alisema kelele zina athari kubwa kwenye afya ya binadamu na mazingira, ikiwamo kukosa ufanisi wa kazi kwa wanaoathiriwa na kelele hizo.

"Kelele zinasababisha watu washindwe kulala na akishindwa kulala, anashindwa kufanya kazi zake za siku kwa sababu anakuwa hajapata usingizi vizuri, wanafunzi wanashindwa kusoma, wazee wanaathirika.

"Tumekuwa tukipokea malalamiko mengi sana. Tukiyachambua hayo malalamiko ya kelele, mengi ni kutoka kwenye baa na nyumba za ibada, kiasi ni kutoka kwenye viwanda hasa vile vinavyotumia teknolojia ambazo siyo nzuri," alisema.

Meneja huyo alifafanua kuwa malalamiko hayo wamekuwa wakiyapokea kwa kiwango kikubwa na kwamba juhudi za kutatua zimeendelea licha ya kupata ugumu kwa wamiliki wa baa na kumbi za starehe kutozingatia sheria. "Sheria ambazo zimewekwa kusimamia masuala ya kelele na mitetemo ni Kanuni za Usimamizi wa Mazingira, Kelele na Mitetemo ya Mwaka 2015," alisema.

Meneja huyo alisema kanuni hizo zimeweka viwango vya juu vinavyoruhusiwa kuzalisha kelele.

"Viwango hivi vimewekwa kulingana na maeneo mahsusi na muda, muda wa mchana kuanzia saa 12 asubuhi hadi saa nne usiku na muda wa usiku unaanzia saa nne usiku na kuendelea hadi saa 12 asubuhi.

"Hivyo, viwango vimetofautina kulingana na muda, lakini pia kuna maeneo kama ya shule, chuo na maeneo tofauti, maeneo ya kazi, maeneo ya biashara," alisema.

Alitoa mfano viwango vya sauti vya juu katika shule na vyuo ni decibel (kizio cha kupima kiwango cha sauti) 45 kwa mchana na 35 kwa usiku huku kwenye makazi ni 50 kwa mchana na 35 kwa usiku.

"Hivi viwango vimewekwa kwa kila anayezalisha kelele anatakiwa kuzingatia hivyo viwango na sheria inamtaka ni wajibu wake kujua kuwa amezidisha au yupo ndani ya viwango kwa maana ya kwamba anatakiwa kuwa na vipima sauti, anatakiwa kujua kama anaendana na matakwa ya sheria," alisema.

Alisema kuwa kutokana na tatizo hilo, upo mwongozo wa kusimamia kelele na mitetemo ambao ulizinduliwa Septemba 2021.

Alitoa wito kwa kila mdau anayehusika kusimamia mwongozo huo, awajibike kwa majukumu yake yaliyoainishwa.

Meneja huyo alisema kumekuwapo na usimamizi dhaifu hasa kwa wanaotoa leseni kwenye kumbi za starehe.

"Watoa leseni wasimamie masharti yanayoendesha hizo shughuli kama ni baa ambayo inatoa sauti nje imepewa muda wa kufanya kuanzia mwisho ni saa sita usiku, lakini ufuatiliaji wa masharti ya leseni umekuwa ni mdogo sana.

"Kwa hiyo, nihimize mtoa leseni asimamie masharti yanayoendana na leseni ili kelele na mitetemo idhibitiwe kwenye nchi yetu," alisema.

Mkuu wa Idara ya Mazingira kutoka Halmashauri ya Mtwara Mikindani, Masumbuko Mtesigwa, alisema watahakikisha wanasimamia sheria na taratibu zilizowekwa ili wamiliki wa kumbi za starehe na nyumba za ibada wazingatie viwango vya sauti zinazotakiwa.

Kanuni za Usimamizi wa Mazingira za Mwaka 2015 zinatoa adhabu ya faini ya Sh. milioni moja au kifungo kisichozidi miezi sita sambamba na kufungia biashara husika.

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu wa ACT Wazalendo, Ado Shaibu (wa tatu kulia), akiendesha harambee ya kukusanya michango ya kuiwezesha Ngome ya Wanawake wa chama hicho Mkoa wa Dar es Salaam jana, baada ya kuzindua Operesheni ya Usajili wa ACT Kiganjani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ‘Moshi mweupe’ gesi asilia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MOSHI ni mweupe! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya jana Rais Samia Suluhu Hassan kutangaza kuwa kesho serikali itatia saini makubaliano ya awali kwa ajili ya kujenga mradi wa gesi asilia (LNG) ambao aliahidi makandarasi wa ndani watashiriki kwa kiasi kikubwa.

Mradi huo unatajwa kuwa unatarajiwa kugharimu Dola za Marekani bilioni 30, sawa na Sh. trilioni 70 za Kitanzania.

Rais Samia alitangaza mpango huo wa serikali jana jijini hapa alipopiga simu katika Kongamano la Makandarasi na Wahandisi wa Miundombinu kumpongeza Rais kwa mchango wake kwenye kuimarisha makandarasi wa ndani.

Rais Samia aliwataka kujipanga ipasavyo kwa kuwa miradi mikubwa inayokuja ni mingi.

“Tutasaini LNG keshokutwa (kesho) na katika ile local content (wawekezaji wa ndani) makandarasi wa ndani tutataka mshiriki kwa kiasi kikubwa ili kukuza uwezo wenu na uchumi wa nchi. Niwaahidi serikali itaendelea kushirikiana nanyi,” Rais alisema na kuamsha shangwe kwa wadau hao.

Aliwatangazia neema makandarasi na wahandisi kuwa wataendelea kupewa kazi mbalimbali kwenye miradi mikubwa na kuwataka kuwa wazalendo.

“Niwaahidi kwamba tutaendelea kujenga sekta ya makandarasi wa ndani kwa kuwapa kazi mbalimbali zinazofanyika ndani ya nchi lakini pia kuwajengea uwezo.

“Lakini niombe makandarasi mjue kazi zinazofanyika ndani ni za nchi yenu, muendelee na uzalendo katika kuzifanya hizo kazi vile inavyotakiwa,” Rais Samia aliagiza.

Alisema makandarasi wa ndani wakipewa kazi nyingi, uchumi wa ndani utakua na kuwapo kwa mzunguko wa fedha.

“Tumelijaribu hilo kwenye fedha za Covid (Uviko-19), kazi imeenda vizuri na ninatumai makandarasi mlifaidika kidogo, jinsi tunavyokwenda serikali itakuwa karibu zaidi na makandarasi na tutahakikisha hizi kazi ndogo ndogo hata miradi mikubwa inayokuja, basi makandarasi wetu wapate kazi kwenye miradi hiyo,” alisema.

# Ujenzi wa vituo vya afya wawatia kitanzini ma-DED

**Na Augusta Njoji,** CHEMBA

WAKURUGENZI wa Halmashauri nchini ambao wapo nyuma katika ujenzi wa vituo vya kutolea huduma za afya wamepewa wiki moja kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, alitoa agizo hilo jana wilayani Chemba mkoani Dodoma baada ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuzungumza viongozi wa wilaya hiyo.

Aliagiza wakurugenzi hao kukutana na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Prof. Riziki Shemdoe, wajieleze kwanini ujenzi huo unasuasua.

“Katibu Mkuu ndani ya wiki moja zile halmashauri ambazo ziko nyuma kwenye ujenzi wa miundombinu uwe umeshakaa na wakurugenzi hawa na waniambie ni kwanini nisiwachukukie hatua kwa wale ambao wako nyuma kwenye ujenzi,” aliagiza.

Bashungwa pia aliagiza wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa kuhakikisha ujenzi wa miundombinu hiyo unakamilika kwa asilimia 100 ifikapo Juni 30 mwaka huu.

“Maelekezo niliyoyatoa ya Juni 30 lazima tukamilishe ujenzi, wakuu wa mikoa na ma-RAS (makatibu tawala wa mikoa) wahakikishe wanasimamia maelekezo haya,” aliagiza.

Aliongeza: “Kabla ya kufikia muda huu ninatarajia kufanya kikao na wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa ambao watatakiwa kutoa taarifa ya hatua walizofikiwa.”

Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kufika Juni 30 mwaka huu kukamilisha miradi ambayo ilikuwa ikitekelezwa kabla ya operesheni maalumu ya UVIKO-19.

Miradi hiyo ni pamoja na kumalizia ujenzi wa hospitali 68 zilizoanza kujengwa mwaka 2018/19, ujenzi wa hospitali mpya 28, kuendeleza hospitali 31, vituo vya afya vipya 354, kuendeleza vituo vya afya 52 na kukamilisha zahanati 763.

**MGOGORO CHEMBA**

Katika hatua nyingine, Waziri Bashungwa ameonyesha kukerwa na migogoro wilayani Chemba ambayo inachangia kuwapo kwa wimbi la watumishi kuomba uhamisho.

“Hapa Chemba mnapata sifa ya kuwa na migogoro kila siku na kama mnavyofahamu kwenye migogoro maendeleo hayawezi kufanyika kwa weledi.

“Sitarajii wana Chemba kuwa mnataka na sifa hiyo, kuna mivutano na watu kugombana pia, sababu ya pili ni wimbi kubwa la watumishi wa halmashauri hii kuomba uhamisho.

“Ningekuwa ninatoa vibali kutokana na kasi ya watumishi wanavyotaka kuhama mtabaki viongozi, mheshimiwa utaweza kufundisha hapa shuleni kama walimu wataondoka? Mheshimwa DC unajua kushika chaki? Ninaamini tutakaa kama watu wazima kujua tatizo nini, kama tutaruhusu uhamisho, hakuna matumishi atabaki,” alionya.

Mkuu wa Mkoa, Anthony Mtaka, alisema ni vyema Halmashauri ya Chemba kuangalia namna ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa hospitali kwa kujenga usiku na mchana.

# ACT: Tuongeze viwango fidia athari wanyamapori

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha ACT Wazalendo kimeitaka serikali iweke viwango vipya kwa ajili ya waathirika wa matukio ya ajali au majanga yanayohusisha wananchi na wanyamapori kwa kuzingatia hali halisi ya maisha na thamani ya uharibifu pamoja na madhara yaliyotokea.

Mbali na hilo, chama hicho pia kimeitaka serikali kuweka wazi hatua zilizofikiwa katika kurejesha masalia ya mjusi mkubwa aina ya Dinosour yanayoonyeshwa katika Makumbusho ya Elimu Viumbe ya Naturkunde Berlin, Ujerumani.

Kauli hiyo ilitolewa na Juliana Mwakang’ali, Msemaji wa Sekta ya Maliasili na Utalii, alipobainisha mambo saba muhimu kwenye eneo hilo la maliasili na utalii.

Mwakang’ali alisema uzoefu unaonyesha kuwa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori hutokea pindi wanyamapori wanapoharibu mali za wananchi (mashamba, mazao, mifugo na makazi) au kuwaua watu, pamoja na watu kutaka kuwaua wanyama hao kwa lengo la kujihami na kulinda mali zao.

“Kwa upande wa fidia, kumekuwapo wa viwango vidogo vya fidia (vifuta jasho na machozi) za uharibifu unaofanywa na wanyama hao kama vile tembo, simba, fisi na chui. Viwango vya sasa kwa mujibu wa kanuni ni Sh. 200,000 hutolewa kwa aliyepata majeraha yasiyo ya kudumu na Sh. 500,000 kwa majeraha au kilema cha kudumu huku wakitoa kifuta jasho cha Sh. 100,000 kwa ekari kwa wale ambao mazao yao yameharibiwa na wanyama pori na Sh. 1,000,000 kwa mwananchi aliyeuawa na wanyama,” alisema.

Kuhusu kurejesha masalia ya mjusi mkubwa, Mwakang’ali alisema ni miaka mingi imepita tangu Watanzania wadai masalia ya mjusi huyo kurejeshwa nchini kwa ajili ya kulinufaisha Taifa, huku kukiwa hakuna juhudi zozote zinazofanywa kuhakikisha masalia hayo yanarejeshwa.

Aliongeza kuwa taarifa za kitaalamu zinaonyesha kuwa asilimia 60 ya mjusi huyo ni masalia halisi kutoka Tendaguru, Tanzania na asilimia 40 ni malighafi za kibunifu kwa ajili ya kupata umbo halisi la mjusi.

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 68/2022**
**In the matter of the Estate of the late THOMAS JOSEPH MTEI of ILAZO within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY FREDERKA ABIUDI SHIRIMA**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **06 Day of June, 2022**
**Date at Dodoma this 10TH day of May, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha MJINI, Mkoa MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi Na. 25/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU AJUZA HAMOUD MSELEM wa MAFIGA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AZIZA SALUM KHALFAN**

**TANGAZO**
(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 Mwezi 06 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imtolewa leo tarehe 23 mwezi 5 mwaka 2022.**

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

# Serikali yasema sekta utalii sasa imefunguka

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana ameihakikishia dunia kuwa sekta ya utalii nchini na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) sasa imefunguka baada ya kupungua kwa janga la UVIKO-19, akihimiza kuvitembelea vivutio vilivyopo.

Akifungua maonyesho ya kimataifa ya Utalii ya Karibu Kili Fair kwa niaba ya Waziri Chana jijini hapa juzi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, alisema kwa sasa masharti ya janga hilo yamepungua na maeneo mengi yanafikika kiurahisi.

"Maonyesho haya yatasaidia kuitangazia dunia kuwa sasa utalii umefufuka tena kwa Tanzania na nchi za EAC na ninatoa wito watu wote mtembelee vivutio vilivyopo," alisema.

Alisema utalii ulipitia purukushani nyingi na kwa sasa hali yake inarudi baada ya kupungua kwa janga hilo na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mstari wa mbele kutangaza vivutio hivyo kupitia filamu ya Tanzania The Royal Tour.

Pia alipongeza waandaaji wa maonyesho hayo ambayo yamekutanisha wadau wa utalii wa nchi za EAC na duniani kwa lengo la kumuunga mkono Rais Samia kutangaza vivutio vilivyopo.

Alisema endapo kila mmoja atashiriki kutangaza vivutio hivyo, sekta hiyo itakuwa na manufaa kwa kila mmoja pia.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahim Bhaloo, alisema kwa sasa Tanzania na nchi za EAC zipo tayari kupokea watalii na wameshaweka mazingira rafiki kwao ikiwamo kuimarisha usalama kwa wageni watakaotembelea kwenye nchi hizo.

"Tanzania Bara kuna utalii wa mbuga na Zanzibar kuna utalii wa bahari kupitia fukwe zake, lakini pia tunashukuru Rais Samia kupitia filamu yake ya The Royal Tour tumeanza kupokea wageni maarufu duniani na maonyesho haya yataongeza idadi ya wageni zaidi," alisema.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kili Fair, Dominic Shoo, ambao ndio waandaaji wa maonyesho hayo, alisema kuwa mwaka huu wamepata washiriki zaidi ya 8,000 kutoka nchi mbalimbali duniani.

Aliomba Watanzania kushiriki katika maonyesho hayo ambayo kuna mengi ya kujifunza kupitia semina zinazotolewa.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, alisema mkoa huo umejipanga kupokea watalii na wanazidi kuimarisha usalama kwa wageni wanaotembelea vivutio vyao.



Mkurugenzi wa Asasi inayojishughulisha na Utu na Mazingira ya HUDEFO, Sara Pima (kushoto), akishiriki kufanya usafi katika ufukwe wa Bahari ya Hindi, eneo la Mbezi Beach Rainbow, mkoani Dar es Salaam jana, wakati wadau wa mazingira wakishirikiana na Manispaa ya Kinondoni na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), waliposafisha ufukwe huo, kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. **PICHA: JENNIFER GILLA**

# 'Watanzania wawajibike kutunza mazingira yao'

**Na Jenifer Gilla**

MENEJA wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda Mashariki, Arnold Mapinduzi, amesema Watanzania wanatakiwa kujitambua na kuwajibika katika utunzaji wa mazingira kwa kuwa sera na sheria ya miongozo ya mazingira ipo.

Alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati baraza hilo liliposhirikiana na wadau wa mazingira na Manispaa ya Kinondoni kufanya usafi katika fukwe za Rainbow katika kuadhimisha Siku ya Mazingira inayofanyika Juni 5 kila mwaka ambapo kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Tanzania ni Moja Tunza Mazingira'.

"Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kifungu namba nne kinasema kila mtu anayeishi Tanzania ana haki ya kuishi kwenye mazingira salama.

"Kifungu cha 6 kinatoa wajibu wa kila mmoja kuhakikisha kwamba mazingira yanasimamiwa na yanatunzwa, kwa hiyo tusipoanza sisi tusitegemee kwamba kuna mwingine atafanya," alisema Arnold.

Aliwataka wakazi wa eneo hilo kutowanyamazia watu wanaochafua mazingira katika ufukwe huo kwa kutupa taka bali watoe taarifa katika maeneo husika ili kukomesha tabia hiyo.

"Ukiona mtu anatupa taka na umemwambia akakudharau, katoe taarifa katika ngazi husika, ukiona ngazi hiyo hawachukui taarifa, nenda ngazi ya juu yake hata ikiwezakana kuja kwetu, wewe njoo na sisi tutafanyia kazi," alisisitiza Arnold.

Ofisa Mazingira wa Wilaya ya Kinondoni, Mohamed Msangi, alisema usafi huo ni mwendelezo wa shughuli zilizokuwa zinafanyika tangu Juni Mosi mwaka huu za kuhamasisha usafi kuanzia kwenye familia, mitaani, masoko na hospitalini na kuwa shughuli hiyo bado itaendelea mpaka pale watakapojiridhisha na hali ya usafi katika manispaa hiyo.

"Manispaa ya Kinondoni tumejaaliwa kuwa na fukwe nyingi, hivyo tunajiongezea nafasi ya kutembelewa na watalii zaidi. Kwa hiyo, kampeni hii ya usafi sisi kama manispaa tutahakikisha haiishii hapa mpaka pale tutakapojiridhisha na hali ya usafi katika fukwe zetu," alisema.

Akiwakilisha wadau wa mazingira, Sara Pima, Mkurugenzi wa Asasi ya Utu na Mazingira (HUDEFO), alisema pamoja na kufanya usafi katika eneo hilo, wameitumia siku hiyo kujadili na viongozi wa serikali ili kujua ni kwa namna gani watatunza mazingira ya eneo hilo ili kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan za kutangaza vivutio na uchumi wa bluu.

"Kama unavyoona hapa leo viongozi wa manispaa na NEMC pamoja na wadau wengine wametuunga mkono. Kwa hiyo, tutajadili mipango endelevu ya kuweka fukwe hizi katika hali ya usafi ili tusirudi kule tulikotoka," alisema Sarah.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mbezi A, Stephen Kinyota, aliwashukuru wadau hao kwa kuwa pamoja nao katika kusafisha fukwe hizo kwa kuwa mchango wao umesaidia kwa kiasi kikubwa kurudisha hadhi ya fukwe hizo.

"Hapo awali fukwe hizi zilikuwa na hali mbaya, uchafu ulitapakaa kila mahali. Kwa kweli hakukuvutia kwa masuala ya utalii, lakini wadau hawa wamefanya kazi kubwa ya kusafisha fukwe hizi kwa miezi kadhaa sasa, tunawashukuru sana," alipongeza.

Aliwataka wakazi wa mtaa huo kuendelea kujitokeza kufanya usafi hata baada ya maadhimisho hayo kwa kuwa bado kuna uchafu mwingi wa kuondoa na kuwa walinzi kwa wale wanaochafua mazingira ili kutorudisha hali ya uchafu iliyokuwapo awali.

Dotto Renatus, mwanafunzi kutoka Chuo Kikuu Dar es Salaam (UDSM), alisema waliungana na wadau hao wa mazingira kufanya usafi ili kuunga juhudi za serikali katika mkakati wa kutunza mazingira ili kuleta hewa safi kwa nchi na pia kuhamasisha vijana kuungana na taifa kuweka mazingira safi.

Joyce Massawe, Mkazi wa Mtaa wa Mbezi A, alisema wamekuwa na utaratibu wa kusafisha fukwe hizo kila Jumamosi kwa kushirikiana na wadau hawa wa kuhakikisha zoezi hilo linakuwa endelevu.

"Nikiwa kama mwenyekiti wa kamati ya mazingira wa mtaa huu, nitahakikisha suala la kusafisha mazingira linakuwa endelevu, hata kama hawa wadau hawatakuwapo.

"Kazi walioifanya ya kutuhamasisha kufanya usafi ni kubwa na kilichobaki ni sisi kuendeleza huo utamaduni," alisema.

Kilele cha maazimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ni leo ambapo kitaifa yatafanyika Dodoma na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Mkuu, Kassim Majaliwa.

# RC aonya viongozi kudhulumu wakulima

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amesema hatosita kuwachulia hatua za kisheria viongozi wa vyama vya msingi (AMCOS) wanaodhulumu wakulima wa pamba na kusababisha kundi hilo kurudi nyuma kimaendeleo na baadhi yao kukata tamaa ya kulima zao hilo.

Mrindoko alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua msimu wa mauzo ya pamba uliofanyika katika Kijiji cha Mnyamasi, Kata ya Ugala huku akitaja matarajio ya mkoa kwa msimu uliopita katika kilimo cha pamba.

Alisema takwimu za mkoa zinaonyesha tangu walipoanza kulima zao hilo mwaka 2017, makadirio yamekuwa yakiwekwa mwaka hadi mwaka ambapo mwaka 2021/22 matarajio yalikuwa kulima ekari 44,955 na matarajio ya mavuno ni kilo milioni 12.

“Miaka iliyopita tuliwahi kupokea malalamiko makubwa ya kwamba baadhi ya viongozi wasio waaminifu katika AMCOS zetu wanapokea pamba ya wakulima, wanapima halafu kuna vile vipointi pointi vile mkulima hapewi,” alisema.

Mrindoko alisema endapo wakifanikiwa kuvuna kwa kiwango tarajiwa, watakuwa wameongeza mavuno zaidi ya mara tano kwa msimu uliopita.

Mkurugenzi wa Kiwanda cha Pamba cha NGS, Daud Silanga, aliwahakikishia wakulima soko la uhakika huku akisema pamba wanayolima ni jasho lao, hivyo lazima walipwe na malipo hayo yatafanyika kwa wakati.

Mwakilishi wa Bodi ya Pamba Mkoa wa Katavi, Joseph Nyesse, aliwataka wakulima kulinda ubora wa pamba kwa kuuza pamba isiyokuwa na uchafu, mawe na mchanga.

Ofisa Kilimo Halmashauri ya Nsimbo, Paul Sheyo, alisema kutokana na wingi wa wakulima wa kutaka kuuza pamba yao, wameongeza vituo vya kuuzia pamba kutoka vituo 20 vya mwanzo hadi vituo 22 vitakavyotumika msimu huu.

Baadhi ya wakulima wa zao hilo waliiomba serikali kuhakikisha dawa wanayoleta ya kuua wadudu wakati wa kilimo cha zao hilo inaendana na eneo husika kutokana na baadhi ya dawa hizo kutofanya kazi na hivyo kusababisha wakulima kupata hasara.

# Askari polisi mbaroni kwa tuhuma mauaji

**Na Idda Mushi,** MOROGORO.

ASKARI wawili wa Kituo cha Polisi Mvuha wilayani Morogoro wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za mauaji ya mkazi na mkulima wa Mvuha, Hamis Hassan (30), maarufu Ng'ombe, aliyepigwa risasi mbili kwenye mguu wa kulia.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Muslim, aliwataja askari hao juzi kuwa ni mwenye namba G8808 D/CPL Mapalala na namba G8626 D/CPL Patrice.

Kamanda Muslim alisema mauaji hayo yalitokea Mei 31 mwaka huu majira ya saa 8.30 mchana katika Kijiji cha Bwila Juu, Kata ya Serembala, Tarafa ya Mvuha wilayani Morogoro.

Alibainisha kuwa siku ya tukio, mwanamke mmoja Scholastica Mathias (29), mfamasia na mkazi wa Mvuha, alikwenda kituoni huko kutoa taarifa juu ya shamba lake alilolima zao la ufuta kuharibiwa kwa kufyekwa na mtu aitwaye Hamis Hassan ambaye inadaiwa walikuwa na uhusiano wa kimapenzi.

Alisema inadaiwa wakati wa uhusiano huo, mtuhumiwa alitoa fedha Sh. 100,000 ili kukodisha shamba na kulima ufuta ambapo baada ya kulimwa, uhusiano wa wawili hao ulivunjika na kuacha mgogoro wa kugombea ufuta.

“Watu hawa walifikishana kwenye ngazi mbalimbali za uongozi wa kijiji na kata kwa nia ya kutafuta suluhu bila mafanikio hadi Mei 31 mwaka huu mmoja wapo alipokwenda kuripoti polisi tukio la kuharibu mali na kufunguliwa jalada,” alisimulia Kamanda Muslim.

Alisema baada ya taarifa hizo, Mkuu wa Kituo cha Polisi Mvuha (hakutaja jina lake), aliwatuma askari hao wawili kwenda kumkamata mtuhumiwa wa tukio hilo la uharibifu wa mali na walipotoa taarifa kwa Ofisa Mtendaji wa Kata (hakutaja jina lake) kuhusiana na sababu ya wao kufika kijijini huko, waliongozana naye kwa kutumia pikipiki yake kwenda eneo la mtoa taarifa.

“Askari Mapalala alibeba silaha aina ya AK47 yenye namba 5002573 kifuani na waliondoka na kwenda eneo la mtoa taarifa Sholastica ambaye pia ni mfanyabishara wa dawa baridi za binadamu.

“Walipokaribia dukani, Koplo Mapalala alishuka kwenye pikipiki na kuzunguka nyuma ya nyumba yenye duka, na wenzake - mtendaji na Koplo Patrice walidhani amekwenda kujisaidia.

“Baada ya muda walisikia milio ya risasi na kwenda kuona kilichotokea na kukuta Hamis amelala chini akiugulia maumivu akiwa na majereha sehemu ya chini ya goti la mguu wa kulia,” alisimulia Kamanda Muslim.

Inadaiwa Koplo Mapalala alizunguka nyuma ya nyumba kutafuta mawasiliano ya simu lakini alimkuta Hamis akiwa na wenzake na Hamis alipomwona askari, alijua anatafutwa ili kukamatwa kutokana na kesi iliyofunguliwa dhidi yake na Scholastica na kuanza kukimbia.


“Alipokimbia umbali wa kama mita 200 Koplo Mapalala alianza kumkimbiza na kufyatua risasi moja hewani akimtaka asimame lakini Hamis aliendelea kukimbia zaidi.

“Alipofika umbali wa mita 250 na akiwa umbali wa mita kama nane kabla ya askari kumfikia, askari alifyatua risasi na kumpiga mguu wa kulia na kudondoka chini ambapo alitokwa damu nyingi na kukimbizwa hospitalini ambako alifariki dunia wakati akipatiwa matibabu,” alifafanua zaidi.

Kamanda huyo alisema mwili wa marehemu ulifanyiwa uchunguzi wa daktari na tayari umezikwa huku jalada la uchunguzi likiwa limefunguliwa dhidi ya askari hao wawili ambao wanashikiliwa na polisi kwa mahojiano zaidi kuhusiana na tukio hilo.

Juzi Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (THBUB) imesema katika uchunguzi ilioufanya, imebaini kupigwa na kuteswa kwa watuhumiwa wakati wa ukamataji ama wakati wa upelelezi kwa madhumuni ya Jeshi la Polisi kupata taarifa zinazohusu matukio ya uhalifu.

Kadhalika, THBUB imebaini askari polisi wanaopatikana na hatia kupewa adhabu isiyowiana na kosa husika alilolifanya ikiwamo kusababisha mauaji dhidi ya watuhumiwa.




Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Mweli (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania Plc, Sitholizwe Mdlalose (kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa Mwananchi Communications Ltd, Bakari Machumu (kushoto) na Mkuu wa Idara ya mambo ya intaneti na akili bandia wa Vodacom, Yvonne Bayona, wakiwa wameshika mfano wa hundi ya Sh. milioni 100, iliyotolewa na kampuni ya Vodacom kwa Mwananchi, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia kuwaunganisha wakulima nchini na mpango wa ‘Farm Clinic’ ili kupata taarifa za kilimo kidijitali na kusaidia wakulima kufanya malipo kwa kutumia M-Pesa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Habari za Sensa ya Watu na Makazi kuingizwa EJAT 2022

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT) limetangaza kuwa katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) 2022, kutakuwa na kundi jipya la Habari za Sensa ya Watu na Makazi.

Kajubi Mukajanga, Mwenyekiti Kamati ya Maandalizi ya EJAT 2022, katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana, alibainisha kuwa kuongezwa kwa kundi hilo kunafuatia maelekezo ya serikali yaliyotolewa Mei 28 mwaka huu wakati wa kilele cha EJAT 2021 jijini Dar es Salaam, ambapo Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa alikuwa mgeni rasmi.

“Kuongezwa kwa kundi hili katika mashindano ya waandishi ni mojawapo ya juhudi za wadau wa habari kuiunga mkono serikali katika kuleta maendeleo ya nchi.

Waandishi wa habari wanatarajiwa kuandika habari zitakazohusiana na Sensa ya Watu na Makazi kwa umakini ili sio tu kuweza kushinda tuzo, bali pia kutoa mchango mzuri kwa mafanikio ya zoezi hilo la kitaifa.

“Hivyo, tunawahimiza wahariri kutumia fursa hii kuhamasisha waandishi kuandika habari zenye kuchagiza mafanikio ya zoezi hili la kitaifa, ikiwa ni pamoja na kufanya uchambuzi na kutumia data,” alisema.

Mwenyekiti huyo aliendelea kubainisha kuwa tuzo za EJAT 2022 zinatarajiwa kuzinduliwa Septemba mwaka huu, zikifanyika kwa mara ya 14 toka zilipoanzishwa mwaka 2009.

Kamati ya Maandalizi ya EJAT inaongozwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na washirika wake ambao ni pamoja na Mfuko wa Vyombo vya Habari Tanzania (TMF), Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika - Tawi la Tanzania (MISA-TAN), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), HakiElimu, Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) na Twaweza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taasisi serikali zijifunze kutoka Wizara ya Ardhi

**WIZARA** ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, jana iliandaa mkutano wa wahariri wa vyombo vya habari mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya kueleza shughuli inazofanya pamoja na kujengeana uwezo juu ya masuala mbalimbali yanayohusu ardhi.

Katika mkutano huo viongozi wote wa ngazi ya juu wa wizara - Waziri Dk. Angelina Mabula, Naibu Waziri Ridhiwani Kikwete, Katibu Mkuu, Dk. Allan Kijazi na Naibu Katibu Mkuu, Nichalous Mkapa, walihudhuria.

Pia wakurugenzi wote na wasaidizi wao katika idara mbalimbali wakiongozwa na Kamishna wa Ardhi, Mathew Nhonge na Mthamini Mkuu wa Serikali, Evelyne Mugasha, walihudhuria. Sambamba na hao, makamishna wa ardhi wasaidizi kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Pwani walikuwapo. Mkutano huo uliokuwa wa aina yake mada kuhusu shughuli za wizara na Sensa ya Majengo na Urasimishaji zilitolewa, hivyo kuwapa wahariri na wanahabari waandamizi nafasi ya kujifunza kwa kina masuala mbalimbali kuhusu sekta ya ardhi.

Aidha, wahariri walipata nafasi ya kuuliza maswali mbalimbali pamoja na kueleza kero zinazoikabili jamii katika sekta ya ardhi huku baadhi wakieleza changamoto zinazowakumba pamoja na baadhi kupatiwa ufumbuzi papo kwa hapo.

Pia wajumbe, kwa maana ya viongozi na maofisa kutoka wizarani kwa upande mmoja na wahariri kwa upande wa pili, walikubaliana kwamba waimarishe daraja la ushirikiano kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata elimu kwa kina kuhusu masuala yanayohusu ardhi na maendeleo ya makazi.

Waziri Mabula na Katibu Mkuu Kijazi, kwa nyakati tofauti walisisitiza kwamba vyombo vya habari ni kiungo muhimu katika kuhabarisha umma juu ya masuala mbalimbali, yakiwamo ya ardhi, hivyo ushirikiano huo ni muhimu na ni wakati muafaka kuuendeleza na kuuimarisha. Wahariri nao waliweka bayana kwamba jambo hilo ni jema katika kudumisha ushirikiano kwa maslahi mapana ya taifa.

Jambo ambalo lilifurahisha zaidi katika mkutabno huo ulioandaliwa kwa pamoja kati ya wizara na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) hakuna kiongozi wala ofisa wa wizara aliyethubutu kutoka tangu kuanza kwake. Hata Waziri aliyekuwa mgeni rasmi katika ufunguzi, aliomba udhuru kwamba angeondoka baada ya kukaa kwa muda fulani lakini hakuondoka. Kitendo cha viongozi hao kukaa hadi mwisho kimeonyesha dhahiri kwamba wamedhamiria kufanya mabadiliko makubwa katika sekta ya ardhi ikiwamo kumaliza migogoro ambayo imetamalaki maeneo mbalimbali. Sambamba na hilo, waliweka bayana kwamba suala la elimu ni muhimu kupitia vyombo vya habari wananchi wengi watapata uelewa mpana kuhusu sekta hiyo muhimu kwa maisha ya kila siku ya mwanadamu.


Waziri Mabula na timu yake wameonyesha kwa vitendo kuwa wamejenga timu yenye ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yao kwa uvumilivu waliouonyesha wa kuhudhuria hadi mwisho bila kuomba hata udhuru. Hata wakati wa kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza, walionyesha wako kitu kimoja na ni watu wenye kuheshimiana bila kujali nafasi zao.

Kwa mfano ulioonyeshwa na viongozi wa wizara hii, wizara zingine na taasisi za serikali hazina budi kuiga na kutekeleza kwa maslahi na maendeleo ya sekta zinazosimamia na taifa kwa ujumla.

Tunasema hivyo kwa sababu katika shughuli za baadhi ya wizara na taasisi za umma, viongozi wakuu na wa ngazi za juu wamekuwa wanakuwapo wakati wa kufungua au kufunga tu huku wakiwaacha maofisa kuendesha na matokeo yake baadhi ya maswali au hoja kushindwa kupata majawabu.

Ni wakati mwafaka sasa kwa serikali ya awamu ya sita, kupitia wizara, idara na taasisi mbalimbali, viongozi wake kuiga mfano wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kuandaa vikao kama cha jana na kuanika mambo mbalimbali ambayo wananchi wana kiu nayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wizara ya Kilimo iwakomboe wakulima toka jembe la mkono

Na Sabato Kasika

**KILIMO** kinatajwa kama uti wa mgongo wa taifa kutokana na kwamba, asilimia 80 ya Watanzania wanaishi maeneo ya vijijini wakijishughulisha na kilimo cha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara.

Pamoja na kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa, bado wakulima wanaendelea kutumia jembe la mkono, wengine wakitumia jembe la kukokotwa na ng'ombe, huku wachache wakitumia trekta.

Katika karne hii ya 21 ya sayansi na teknolojia, ninadhani umefika wakati sasa kufanya mapinduzi zaidi kwenye kilimo kutoka cha kujikimu ambacho kinatumia jembe la mkono kwa kutegemea msimu wa mvua hadi cha umwagiliaji na pia kulima kwa kutumia trekta.

Ukweli ni kwamba, jembe la mkono linamuwezesha mkulima kulima eneo dogo tena kwa nguvu kubwa huku akiwa hana uhakika kupata mavuno kutokana na mabadiliko ya tabianchi ambayo wakati husababisha mavuno kukosekana.

Kuna msemo kwamba mchumia juani hulia kivulini lakini kwa kilimo cha jembe la mkono ambacho kimeendelea kutumika tangu nchi ipate uhuru mwaka 1961, ni wazi mkulima anaendelea kuchumia juani na kulia juani.

Hivyo, ninadhani katika karne hii ya 21 tubadili kilimo chetu ili kitusukume kwenda, kwa sababu hakuna kitu kingine cha kutusukuma, isipokuwa kilimo, kwani kilimo ndicho uti wa mgongo wa taifa.

Kimsingi, jembe la mkono kwa sasa siyo rafiki kwa vijana ambao baadhi yao wamekuwa wakikimbilia mijini kujishuhulisha na biashara ndogo ili kujikimu kimaisha, hivyo ipo haja ya kuangalia uwezekano wa kubadili kilimo.

Katika mwaka fedha wa 2022/2023, Wizara ya Kilimo imejiwekea mipango mbalimbali kwa ajili ya kuboresha kilimo nchini, ikiwamo kuimarisha utafiti, kutoa ruzuku za mbegu za alizeti, ngano na miche ya michikichi.

Mbali na hilo, wizara hiyo pia inakusudia kuimarisha upatikanaji wa pembejeo za kilimo, kuimarisha na kutoa huduma ya upimaji wa afya ya udongo, kuendeleza kilimo cha umwagiliaji, ukiwamo ujenzi wa mabwawa ya kuvunia maji ya mvua.

Hayo ni kwa mujibu wa Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe wakati akiwasilisha bajeti ya wizara yake bungeni hivi karibuni akielezea mambo mbalimbali ambayo inakusudia kuyafanya kwa ajili ya maendeleo ya kilimo nchini.

Bashe pia anagusia kuimarisha upatikanaji wa masoko, upatikanaji wa mitaji ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfuko wa maendeleo ya kilimo utakaowezesha upatikanaji wa pembejeo.

Anataja maeneo mengine kuwa ni kuimarisha miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maghala, pia kuimarisha kilimo cha mashamba makubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha maeneo maalum ya mashamba hayo na kutoa ruzuku ya mbolea mwaka 2022/23.

Pamoja na hayo, suala la kuachana na kilimo cha jembe la mkono lingewekewa mkakati ili kuhakikisha wakulima wanaondokana na adha kupitia jembe hilo ambayo ni kutumia nguvu nyingi kulima eneo dogo.

Waziri Bashe katika mipango yake, anasema wizara imepanga kuongeza ajira milioni moja za vijana kwenye sekta ya kilimo ifikapo 2025 kwa kuanzisha programu yao iitwayo 'Build Today for a Better Tomorrow'.

Mazao yatakayozingatiwa katika utekelezaji wa mradi huo ni alizeti, soya, ngano na mazao ya bustani, ambapo Sh. bilioni tatu zimetengwa. Sh. bilioni moja kati yake zitatumika kama dhamana ya mikopo kwao.

Mipango hiyo ni mizuri, lakini kilimo kingewekewa mazingira ambayo ni rafiki hasa kuondokana na jembe la mkono, ili kuvutia vijana wajitokeze kwa wingi kujishughulisha na kilimo badala ya kukimbilia mijini kutafuta kazi.

Nguvu kubwa ikielekezwa kwenye kilimo cha kisasa na kuachana na jembe la mkono ambalo huenda likawa ni kikwazo kwa baadhi ya vijana. Ninaamini wanaweza kujitokeza kwa wingi kushiriki katika shughuli za kilimo.

**SAFU**

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# *Rais Samia ameonyesha ni mkweli na mtu wa vitendo*



**Na Pascal Mayalla**

KWA Wakristo, Bwana Yesu Kristo, kabla ya mateso, kifo chake msalabani, kufufuka kwake na kupaa mbinguni, alituasa kuhusu manabii wa uongo, akasema: "Watakuja watu, watafanya ishara kwa jina langu, watahubiri na kufanya miujiza kwa jina langu, lakini si wangu". Ndipo mmoja katika mkutano ule akauliza: "Je, tutawatambuaje?" Pale pale Bwana Yesu alimjibu "Mtawatambua kwa matendo yao."

Hili ni neno kubwa sana. Bwana Yesu alitufundisha jinsi ya kuwatambua wakweli na wa uongo kupitia kwa matendo yao. Mafundisho haya ya Yesu Kristo ni kwa watu wote. Hata kwa ndugu zetu Waislamu, nawaombeni msijisikie wazito kupokea mafundisho haya kwa kuyaona kama si ya imani yenu. Yesu Kristo huyu wa kwenye Biblia Takatifu, ndiye yule yule Nabii Issa bin Maryam, wa kwenye Quran Tukufu.

Binadamu amepewa uwezo mkubwa wa kujifanyisha na kwa kutumia kauli. Uhusiano na mapenzi huanza kwa kauli "nakupenda". Kwa huku Afrika, ikitokea ni mwanamke anapenda, anachoweza kufanya ni kujipitisha pitisha tu ili aanzwe. Wenzetu wazungu wao wamepiga hatua kidogo. Akitokea ni mwanamke anapenda, analianzisha tu.

Kwa vile neno nakupenda ni kauli tu na mwanamke akishaambiwa nakupenda, wengine warahisi na papo hapo hufungua mioyo yao na kuanza kupenda, hivyo hawezi kujua kama anapendwa kweli au anadanganywa. Mwanamuziki wa Marekani Whitney Huston, aliwahi kutunga wimbo kuuliza hili swali "How Will I Know" sehemu ya maneno ya wimbo huo ni "How will I know if he really loves me?", akimaanisha nitajuaje kama ni kweli ananipenda kwa dhati?

Swali kwa dada zetu, mtu anapokutokea kwa kauli "nakupenda", utajuaje kama anakupenda kweli au anakudanganya tu ili kukutumia? Jibu ni moja tu, kwa matendo yake.

Jibu la kuutambua ukweli kutoka kwenye kauli ni kupitia matendo. Mtu akikwambia nakupenda, ili kumjua kama anakupenda kweli, utambaini kwa matendo yake. Na kwa kulijua hilo, wanaume malaghai wa mapenzi, baada ya kukwambia anakupenda, hufanya pia ulaghai wa matendo kama kukunulia chips kuku na kukuhonga pesa ili tu kuufungua moyo wako umkubalie na kumpa anachotaka. Akiishapata huyo humwoni tena!.

Ugumu huu wa kuujua ukweli wa kauli, umewatesa wengi, kujikuta wameingia kwenye uhusiano wa mapenzi na ndoa zimefungwa, zingine hadi watoto wamezaliwa. Baada ya hapo ndipo unakuja kuujua ukweli wa ulaghai wa mwezi wako kwa matendo kuwa si mkweli. Kwa wanawake majasiri na mashujaa, baada ya kuutambua ukweli, huomba talaka zao na kwa dini ambazo haziruhusu talaka, huishi kwenye ndoa za mateso. Laiti wanawake hawa wangejipa muda wa kutosha kutafakari kwa kuyachunguza matendo ya wenzi wao wala wasingelikubali kuolewa.

Ushauri kwa watoto wa kike na wanawake wote, mwanamume anapokutokea kukwambia anakupenda, kwanza furahi maana kupendwa ni raha, ila usimpe jibu la papo hapo kuwa na wewe unampenda bali mwambia asante, nipe muda. Baada ya hapo tumia moyo wako kujiuliza je, huyu ananipenda kweli, kwa dhati ya moyo wake?. Sauti toka ndani yako, itakwambia ukweli. Fuata hicho roho inachokuambia, hutapotea wala kukosea.

Kama walivyo wanaume malaghai wa mapenzi, hutoa kauli za kilaghai kuwadanganya wenzao ili wapate wanachotaka, ndivyo ilivyo kwa baadhi ya wanasiasa na viongozi malaghai. Hutoa kauli na ahadi kemkem za kuombea kura, kumbe ni kauli na ahadi za uongo. wakishachaguliwa, huwaoni tena, wataibuka baada ya miaka mitano, ule mwaka wa uchaguzi na uongo mwingine na ulaghai mwingine!

Rais Samia Suluhu Hassan baada tu ya kuapishwa, alitoa kauli njema ya maridhiano na kuliponya taifa. Ile haikuwa ni kauli tu, imefuatiwa na matendo. Amefanya matendo mengi makubwa ya kuliponya taifa. Amekutana na wapinzani, akiwemo mpinzani machachari sana Tundu Lissu. Tangu alipopigwa risasi na kulazwa Nairobi kuna watu wakadhani inakatwa kwenda kumpa pole lakini kuna watu majasiri, wenye moyo wa huruma na upendo wa kweli, walikwenda kumjulia hali na kumpa pole bila kuogopa watu.

Chini ya utawala wa Rais Samia, kesi zote ambazo hazikuwa na haki na zingine japo ni kesi kweli zimefutwa kwa ajili ya maridhiano. Licha ya mahakama kumthibitisha Freeman Mbowe ana kesi ya kujibu, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) aliifuta. Kwa vile kwa mujibu wa katiba yetu, mtu pekee mwenye uwezo wa kuifuta kesi ni DPP, hivyo wanaojua aliyefuta kesi ya Mbowe ni DPP, lakini wanaojua zaidi aliyefuta ni nani wanajua.

Mbowe baada tu ya kutoka gerezani alikwenda wapi kusema nini, tunajua.

Wiki hii kwenye mitandao ya kijamii, zimesikika habari, Tundu Lissu amelipwa haki zake zote. Huu ni uthibitisho mwingine kuwa Rais Samia anatenda kile anachokisema.

Naamini kupitia "kikosi kazi", siku chache zijazo Rais Samia ataruhusu mikutano ya siasa, ataifumua na kuisuka upya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa kuifanya iwe shirikishi.

Natamani wema huu wa Rais Samia pia uangazie ubatili fulani ndani ya katiba yetu.

Kwa maana hiyo, mpaka sasa, hapa tulipo, Rais Samia, ameshathibitisha kwa kauli na matendo kuwa yeye ni msema kweli na mtenda kweli, ni msema haki na mtenda haki. Watanzania katika umoja wetu, hatuna budi kumshukuru Mungu kwa kutuletea Samia.

Wema wake unaliponya taifa na kwa matendo haya ya haki, Rais Samia anayoyafanya, atabarikiwa sana na taifa litabarikiwa na kupata ustawi wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Asante Mungu kwa Samia, ni baraka kwa nchi yetu. Swali linabaki moja tu, je, kwa wema wake, atauacha ubatili huu ndani ya katiba yetu?

Ni ubatili gani huo ndani ya katiba yetu?, tukutane wiki ijayo.

**Wasalaam**
**Paskali 0754 270403.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# *Acheni Chifu Hangaya aitwe Hangaya!*



**Na Joseph Kulangwa**

**Yanga alimnyamazisha Simba katika nusu fainali ya soka ya Kombe la Shirikisho la Azam kwa kumbamiza kombora moja kwa nunge. Leo Simba anaugulia lakini hana la kufanya, hivyo naye anasubiri zamu yake.**

UTANI ni hali ya watu au makundi mawili kufanyiana mzaha wa kijadi lakini ulio na staha na chanya kwa pande husika.

Ni dhana ambayo hutumika wakati mwingine kufarijiana kwenye matatizo ikiwa ni pamoja na misiba ambako mara nyingi utani hujitokeza.

Misibani utani hujitokeza pale waombolezaji wanapoamua kubeba gharama na shughuli zote za msiba, huku wakiendelea kuwazodoa wafiwa lakini kwa staha.

Si mara moja au mbili kukuta wafiwa wameviziwa usiku na kusilibwa majivu usoni wakiwa wamelala huku wakizodolewa na kutuhumiwa kuwa wauaji wa ndugu yao.

Lakini yote hayo huwa mzaha au maskhara tu ili kuhakikisha msiba au maombolezo yanakweda bila sonona au matatizo na kumalizika kwa usalama na amani. Hivyo utani una mchango katika kudumisha amani kwenye jamii.

Iko mifano mingi ya utani, kwani siku za karibuni, watani wawili katika tasnia ya michezo walikutana katika uwanja wa soka wa Kirumba, Mwanza ambako mtani mmoja alimnyamazisha mwenziwe.

Yanga alimnyamazisha Simba katika nusu fainali ya soka ya Kombe la Shirikisho la Azam kwa kumbamiza kombora moja kwa nunge. Leo Simba anaugulia lakini hana la kufanya, hivyo naye anasubiri zamu yake.

Mwaka 1995 akizungumza na wanahabari katika hoteli ya Kilimanjaro, Dar es Salaam, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alitoa utani uliowaacha hoi wanahabari ukumbini.

Alisema siku moja alimtuma Hayati Sir George Kahama kwenda Congo, bila shaka ilikuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Akasema Sir George wakati huo alikuwa waziri wake, hivyo alipanda ndege.

Akasema ndege iliporuka, Sir George akashituka na kusema 'Oh My God!', iliporuka juu tena akashituka na kusema 'Mama Yangu!', iliporuka zaidi akashituka tena na kusema 'Maweee!'

Mwalimu alimaanisha jinsi Sir George aliposhituka akijua anakufa, hivyo kumlilia mama yake kwa lugha ya Kiingereza kwanza, ikafuata ya Kiswahili na hatimaye kumalizia na Kihaya.

Sir George alikuwa Mhaya na Wahaya wa Kagera na watu wa Mara ni watani. Ikumbukwe Mwalimu Nyerere alikuwa Mzanaki wa mkoani Mara, hivyo utani kwao ulikuwa jadi yao.

Utaona kwamba utani unafurahisha, unaleta utulivu, faraja na kudumisha amani katika jamii kama nilivyobainisha hapo juu. Hiyo ndiyo sababu utani hauna mashitaka na ukimwahi mtani wako mmalize.

Mtacheka yatakwisha kwa sababu huwa ni rahisi sana mtani kukubali kushindwa kwa sababu hapana gharama kubwa ingawa pia kuna vijigharama vidogo vidogo.

Mathalan, mtani anaweza kukukuta na kitu akakuomba akushikie. Ukijisahau ukampa mkononi, jua imetoka hiyo na ana haki ya kukichukua moja kwa moja na kukimiliki na usimfanye lolote. Huo ndio utani lakini una mipaka yake.

Nayasema haya kwa kuona nchi inavyokwenda chini ya Chifu Hangaya. Kwa kweli anafanya mambo ambayo kwangu mimi nayaona ya ajabu sana katika taifa hili ambalo halikuyazoea.

Hivi nani aliamini kwamba Chifu Hangaya ingetokea siku akahudhuria tamasha la msanii wa kizazi kipya na mbunge wa zamani Joseph Mbilinyi 'Mr Sugu'? Hiyo ikizingatiwa kuwa Sugu ni mwanasiasa wa upinzani ambaye kwa miaka sasa amekuwa mwiba kwa serikali.

Miaka sita iliyopita, tuliambiwa kuwa atakayechagua mpinzani basi asahau maendeleo katika eneo lake. Leo mambo haya hayapo tena, Sugu anakaa meza moja na Rais, Mwenyekiti wa chama kingine, anakaa na Makamu Mwenyekiti wa chama tawala!

Leo Rais, Chifu Hangaya anakubali kuzindua kitabu cha mpinzani! Anampa kiki mpinzani! Leo Rais anamkaribisha kiongozi wa chama cha upinzani Ikulu wanakaa na kuzungumza kama Watanzania!

Upinzani wa kisiasa ni sawa na utani wa jadi kwamba mnazodoana lakini na baadaye maisha yanasonga mbele kwa maslahi mapana ya jamii yenu bila kutafutana ubaya na kuchokonoana hata kutoana damu.

Namwona Chifu Hangaya kama mtu asiye na tamaa ya madaraka, asiye na ujivuni wa madaraka, mtu aliyetosheka na alichonacho, lakini anayetamani na mwingine akipate na aridhike na kuwa Mtanzania, kwamba nchi ndiyo hii na kila mmoja ana haki ya kuishi na kupata riziki yake.

Sijui huko mbele kutakuwaje lakini kwa haki ya Alah namwona Chifu Hangaya kama mwenye maono chanya na nchi hii, lakini anayetaka kuacha alama yake kwa Watanzania kwamba walipata kuwa na kiongozi rahim aliyejali na kupenda watu wake bila ubaguzi. Inshallah!

# Watumishi wa ndani ni baraka au karaha?



BILA shaka watu wengi wamewahi kuishi, kuhudumiwa au kumwona mtumishi wa ndani wa kike au kiume akifanya kazi kwenye familia fulani, kazi ambazo ni jukumu la wanafamilia husika.

Baadhi ya watumishi wamefanyika baraka katika nyumba za waajiri wao lakini wengine wamekuwa tatizo na mzigo. Changamoto za watumishi wa ndani na waajiri wao au familia wanazoishi, zinaongezeka kila siku.

Hivi karibuni vyombo vya habari vimetoa taarifa ya binti ambaye ni mtumishi wa ndani anayedaiwa kumnyonga mtoto wa waajiri wake mwenye umri wa miaka minane, Kimara Temboni, Dar es Salaam, na kumsababishia kifo.

Taarifa ya wazazi wa marehemu kwa vyombo vya habari inaonesha kutomfahamu vizuri mtumishi wao wa ndani kwa sababu ya majukumu yao mengi ya kikazi. Tukio hili la kusikitisha linaweza kuwa angalizo kwa wazazi na walezi wote hapa nchini.

**SABABU ZA KUAJIRI**

Kupata ajali ya gari haimaanishi kutokupanda gari tena. Bado vyombo vya usafiri vinahitajika ili kusafirisha watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kwa mantiki hii, pamoja na udhaifu walio nao watumishi wa ndani, bado umuhimu wao ni mkubwa katika familia nyingi, hasa kwa wale ambao ni waajiriwa, waliojiajiri na wastaafu. Ni ukweli usiopingika kuwa hali hizo zimewasukuma watu wengi kuajiri watumishi wa ndani ili wawasaidie majukumu mbalimbali katika nyumba na familia zao.

Hali kadhalika, wako baadhi ya wanandoa ambao majukumu yao ya kikazi huwafanya kutopatikana nyumbani mara nyingi. Wengine safari nyingi za kikazi na kibiashara ndani na nje ya nchi zimewafanya kutokuwa na muda na nyumba zao, hivyo kulazimika kuajiri watumishi wa ndani.

Kwa upande mwingine, uvivu wa baadhi ya watu umewasukuma kuajiri watumishi wa ndani. Baadhi ya watu ni wavivu kwa asili kwa sababu ya malezi na makuzi mabaya wakati wa utoto. Hawakufunzwa maarifa ya nyumbani na stadi za maisha wangali wadogo. Kwa hiyo, wengi wao wanashindwa kuwajibika na kumudu kazi mbalimbali katika nyumba zao kwa sababu walikuzwa katika hali ya kufanyiwa kila kitu na watu wengine.

Hali hii imesababisha baadhi ya wanafamilia kukabidhi majukumu yote ya nyumbani kwa watumishi wao wa ndani ikiwa ni pamoja na jukumu la malezi ya watoto na kutunza nyumba. Hii imesababisha watoto wengi wa sasa mijini kuwa na malezi ya watumishi wa ndani zaidi kuliko wazazi wao hali inayopunguza thamani ya wazazi kwa watoto wao.

Wazazi wanapokuwa wavivu, huwabomoa watoto wao kimakuzi. Uvivu wa wazazi hutengeneza kizazi cha watu wavivu na wazembe katika familia na jamii. Watumishi wanapoachiwa majukumu yote ya ndani ya nyumba, wengine hujisahau na kujiona wanayo haki ya kumiliki vilivyomo ndani ya nyumba za waajiri wao au kufanya chochote wanachotaka.

**KUKABILI CHANGAMOTO**

Kuzungumzia matatizo tu haisadii, bali ni muhimu kutafuta njia za kukabili matatizo yanapojitokeza ili kuishi kwa amani, furaha na utulivu. Mambo yafuatayo yanapaswa kuzingatiwa ikiwa ni sehemu ya kukabiliana na changamoto za watumishi wa ndani;-

Kwanza, wanandoa wafahamu nafasi na wajibu wao. Uwapo wa mtumishi wa ndani isiwe sababu ya kudumu ya wanandoa kutowajibika katika ndoa. Wanandoa wawe na muda na nyumba zao ili wasiwe wageni na sababu ya majanga katika nyumba zao.

Pili, ni muhimu kuwafahamu vizuri wale unaowaajiri kuwa watumishi wa ndani kwa sababu ni watu ambao muda mwingi zaidi watakuwa nyumbani na watoto wako kuliko wewe mwenyewe. Hivyo, fahamu mahali, familia anayotoka, itikadi za kiimani na historia yake.

**Ni muhimu kuwafahamu vizuri wale unaowaajiri kuwa watumishi wa ndani kwa sababu ni watu ambao muda mwingi zaidi watakuwa nyumbani na watoto wako kuliko wewe mwenyewe. Hivyo, fahamu mahali, familia anayotoka, itikadi za kiimani na historia yake.**

Changamoto ya kutokumfahamu mtu inakuwa kubwa na yenye madhara hasa pale inapozaa matukio ya ajabu na kutisha. Watu wengi wamelizwa na kuumizwa na watumishi wao wa ndani kwa sababu ya kutokuwafahamu vizuri mapema.

Kwa upande mwingine, ufahamu wa mahali na familia anayotoka utakusaidia pale mtumishi mwenyewe atakapopata tatizo linalohitaji mawasiliano ya wewe mwajiri na familia yake. Itakuwa rahisi kwa mwajiri kufikisha taarifa kwa familia yake husika kuhusu mtumishi.

Tatu, watumishi wa ndani waelekezwe majukumu yao kwani yale mwajiri anayotamani yafanyike, inawezekana mtumishi wake hayajui kutokana na mazingira na familia aliyotoka.

Kumekuwa na changamoto kwa watumishi wa ndani hasa pale wanapokuwa hawatambui vizuri majukumu yao katika familia husika. Ni muhimu sana watumishi waelekezwe na kuambiwa cha kufanya na jinsi ya kufanya na wapewe vitendea kazi.

Kuelekeza isiwe jambo la muda mfupi tu, bali liwe endelevu mpaka pale mwajiri atakapojiridhisha kuhusu ubora na utendaji wake ili kukidhi matarajio yake. Watumishi wa ndani wakumbushwe na kukosolewa kwa upole na upendo pale wanapokosea badala ya kutafuta makosa yao tu. Kinyume cha hapo, mwajiri anaweza kujikuta anamtengeneza adui atakayesababisha madhara katika familia yake.

Nne, watumishi wa ndani ni watu wenye hisia kama watu wengine. Wanafamilia wawathamini na kuonesha utu kwa watumishi hawa ili nao wapokee mema yao. Mtumishi anapokosea akosolewe na kusahihishwa kwa staha kwani ndiye anayekusaidia kulea watoto na kutunza nyumba yako. Vinginevyo, hasira yake kwa kuhisi kutokutendewa haki inaweza kusababisha ajenge roho ya chuki na kisasi kwa kudhuru mtoto au watoto ulio nao au wewe mwenyewe au kuharibu mali ulizo nazo.

Kwa mantiki hiyo, ifahamike kuwa si watumishi wote wa ndani ni tatizo. Makala hii ikusaidie wewe msomaji kufahamu kwamba, mtumishi wa ndani anaweza kuwa lango la baraka au karaha katika familia au nyumba yako kutokana na namna alivyopatikana, historia ya maisha yake, malezi na makuzi yake katika familia anayotoka, na jinsi unavyoishi naye. Hekima, busara, uangalifu na umakini vinahitajika sana.

■ **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066]**

**Watumishi wa ndani wakumbushwe na kukosolewa kwa upole na upendo pale wanapokosea badala ya kutafuta makosa yao tu. Kinyume cha hapo, mwajiri anaweza kujikuta anamtengeneza adui atakayesababisha madhara katika familia yake.**

# MAISHA

JUNI 5, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumap




Ukurasa 13

**Malkia Elizabeth mitindo ya mavazi yake hatari**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Umuhimu wa vifaa bora katika ujenzi wa ukuta wa nyumba yako



Ukurasa 12

**HARUSI**




### JING'ARISHE KIPUPWE


# Ngozi ibaki laini wakati wote

Ukurasa 14

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | T | A | M | K | O |
| ■ | A | ■ | ■ | A | ■ |
| U | M | A | ■ | N | ■ |
| ■ | B | ■ | U | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | I | ■ |
| S | A | N | D | A | ■ |


## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




@A.MSAMBA

## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi: AMA, IPO, WINDA, PWANI, NYUMBA, PEPONI

## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa na baba yake wakila chakula cha jioni, siku hiyo alikuwa na furaha sana baada ya mama yake kupika wali na maharage.

Baba yake Juma alikuwa akimtazama mtoto wake jinsi alivyokuwa akila huku akijilamba mkono wake kutokana na utamu wa chakula.

**BABA:** Leo Juma umefurahia chakula hadi unajilamba mkono!

**Juma:** Baba chakula kitamu sana, mama kapika na maharage ya nazi.

**Baba:** Sawa mwanangu endelea kula

**Juma:** lakini baba eti huwezi kuulamba mkono kama hakuna chakula? Ndio maana ya ile methali mkono mtupu haulambwi?

**Baba:** Hapana ule msemo unamaanisha kama huna kitu, si rahisi kusikilizwa na si vingine

**SWALI**

Mlima Meru unapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Ijue siri iliyojificha kwenye fedha kuinua maisha yako

***KARIBU tena msomaji wangu tuendelee kuchambua masuala mbalimbali kuhusu maisha yetu ya kila siku. Leo hebu tujadili kuhusu fedha na siri iliyojificha ndani yake. Pia kwa nini Mungu anatahadharisha tusipende fedha!***

> **"Msiwe na tabia ya kupenda fedha; muwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.**

Fedha au pesa imewagawa watu katika makundi mawili. Moja ni wale wanaopenda fedha, pili, wale wanaohitaji fedha. Wako watu wamefarakana na imani na kujipatia maumivu mengi katika mahangaiko ya kutafuta fedha.

Fedha ina tabia ingawa siyo kitu hai. Ukifanikiwa kujua tabia na mwenendo wa fedha utakuwa umefahamu siri kubwa itakayoweza kukupa mafanikio katika maisha!

Watu wengi wanadhani ukipata fedha za kutosha, matatizo yako yatakwisha nawe utakuwa na maisha ya furaha. Pia wanaamini kuwa fedha ni mwarobaini wa matatizo yote ya mwanadamu.

Mungu alipomuumba mwanadamu, fedha haikuwa moja ya vitu alivyopewa ili kujipatia maisha bora. Fedha ni ubunifu wa mwanadamu ambao alidhani unaweza kurahisisha upatikanaji wa mahitaji yake.

Hata hivyo, akatahadharisha katika maandiko yake kadhaa kwamba tusipende fedha pale aliposema; "Maana shina moja la mabaya ya kila namna ni kupenda fedha; ambayo wengi wangali wakiitamani hiyo wamefarakana na imani, na kujichoma kwa maumivu mengi".

Pia akasisitiza, "Msiwe na tabia ya kupenda fedha; muwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema "Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa".

Fedha kama fedha haina thamani mpaka iambatanishwe na bidhaa. Kwa hiyo tambua siri ya kwanza kwamba fedha huambata na bidhaa, yaani bidhaa ndiyo inayovuta fedha. Na fedha huenda pale tu palipo na bidhaa( bidhaa inajumuisha vitu na huduma).

Hata biashara ya kuuza na kununua fedha huishia kwenye vitu vitakavyo nunulika kwa kutumia fedha. Shida moja kubwa tunayoipata wengi wetu tunapotafuta fedha, ni kule kutaka kupata fedha bila kubadilisha na vitu vitakavyovuta ile fedha unayoitaka.

Hapa nchini tumesikia sana habari za wafanyakazi hewa, malipo hewa, utapeli na kadhalika. Hii ndiyo ile tabia ya kutaka fedha bila kutambua kwamba bila kuambatana na vitu vyenye thamani ni lazima baada ya muda mfupi itakutoroka. Fedha ina tabia na inaweza kutambua wapi iende na wapi isiende!

Ukweli huu unatufanya kujifunza siri ya pili kwa sababu fedha huenda pale palipo na bidhaa. Dhana ya kuweka fedha akiba imepotoka sana na huishia kuwafanya watu wengi kutokuona faida kuweka akiba.

Taasisi nyingi za fedha husisitiza watu kuweka akiba ya fedha na kuahidiwa faida ya riba baada ya muda fulani. Ili fedha iongezeke ni lazima uzalishaji wa bidhaa nao uongezeke. Fedha iliyowekwa akiba haiongezi uzalishaji wa kitu chochote kwa yule aliyeiweka akiba. Ile taasisi ambayo wewe umekwenda kuweka akiba huko wanajua siri hii!

Fedha yako hawaifungii sehemu salama ili ukizitaka uzipate, hapana, wanazikopesha kwa watu watakaozalisha kitu kitakachovuta fedha zaidi. Ndio sababu unapokwenda kukopa fedha benki wanataka uwaonyeshe mchanganuo wa jinsi utakavyokwenda kuzitumia hizo fedha.

Msomaji wangu, ukitaka kufanikiwa katika kuongeza kipato chako, usiweke fedha akiba benki bali ziwekeze mahali ambapo zitazalisha vitu zaidi na wewe kupata fedha zaidi!

Taasisi za fedha unapokwenda kuweka akiba fedha zako wanakuahidi riba ya asilimia mbili au tatu kwa mwaka. Unapokwenda kukopa fedha ulizoweka akiba utatozwa riba asilimia 17 hadi 20. Jiulize, ni nani hapo anayepata faida katika fedha zako ulizoweka akiba?

Kosa moja kubwa tunaloendelea kulifanya wasomi na wasio wasomi ni kutojifunza mwenendo mzima wa fedha. Fedha ndiyo bidhaa moja tunayohitaji sana tuweze kufanikiwa katika maisha yetu. Hata hivyo, hatuna elimu ya kufahamu matumizi yake sahihi!

Ujinga huu umepelekea watu wengi kujitia katika maumivu wanapohangaika kutafuta fedha. Inaelezwa kuwa moja ya shina la uovu hapa duniani ni kupenda fedha. Utakapofahamu vema siri ya fedha hautaendelea kuipenda bali kuihitaji kama nyenzo moja muhimu katika mafanikio yako.

***Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kuhusu siri mbili zilizojificha kuhusu fedha. Wiki ijayo nitakudokeza siri ya tatu ya kuzingatia ili uweze kupata fedha zaidi. Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI
Na Salome Kitomari



# NEMC ichukue hatua kwa vitendo, maneno yametosha

SHERIA ya Mazingira imelipa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) meno ya kudhibiti wanaoivunja. Licha ya nguvu hizo bado tunawasikia wakizungumza na vyombo vya habari kuwaonya wanaovunja sheria.

Mathalani, mara kadhaa na hata wiki iliyopita, wamesema watawashughulikia ipasavyo wenye nyumba za ibada, kumbi za starehe na wengine ambao wamegeuka kuwa kero kwa wananchi kwa kuwa wanaendesha shughuli zao hadi usiku wa manane.

Kwa sasa, kasi ya kufungua baa na kumbi za starehe inaongezeka na mbaya zaidi ni ambazo hazina vifaa vya kuzuia sauti huku zingine zikiwa katikati ya makazi ya watu.

Mathalani, maeneo ya Tabata na Sinza kwa sasa kumekucha kwa kuwa na kumbi za starehe zinazopiga muziki hadi usiku wa manane kiasi kwamba wananchi wanaoishi jirani hushindwa kupumzika, inakuwa nao wako kwenye hizo kumbi kwa kuwa muziki ni mkubwa sana.

Pia nyumba za ibada zinazoendesha mkesha usiku kucha kuanzia Jumapili hadi Jumapili, zinazidi kuongezeka na mbaya zaidi hazizingatii vigezo vya ujenzi ili kudhibiti kelele ambazo ni kero kwa wengine.

Kwa hayo yote tumewasikia NEMC wakitoa onyo kali lakini bado hatujaona watu wa mfano waliokamatwa na kuchukuliwa hatua kali kwa mujibu wa sheria, ili wanapojenga kumbi hizo wazingatie vigezo vyote kwa kuzuia sauti.

Kuna wakati NEMC ilitoa orodha ya kampuni zinazomiliki vituo vya mafuta ambavyo vilijengwa bila kupata vibali vya mazingira, baadhi vilikuwa mjini na vilishaanza kuendesha shughuli.

Swali la kujiuliza ni kwa nini wanafikia kufanya hivi na nani yuko nyuma ya wawekezaji hawa kiasi cha kuidharau mamlaka halali kama NEMC kuanza kazi bila kuwa na cheti cha ukaguzi wa mazingira?

Hii inazidi kuleta wasiwasi juu ya nguvu za NEMC kama inaachwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria,yawezekana mbele tukawaona wao kwamba wameshindwa kukamata au kufungia nyumba za ibada au kumbi za starehe ila kumbe wanavutwa 'shati' kutekeleza wajibu wao.

Ziko familia zimehama nyumba zao kutokana na uwapo wa kumbi na nyumba hizo za ibada. Mtu anatoka nyumbani kwake kwenda kutafuta anarudi hapati muda wa kupumzika na mbaya zaidi nje ya geti lake anakuta wamejaa madada poa wanaojiuza na kufanya ufuska bila woga.

Kwenye nyumba hizo kuna wagonjwa, wazee na wanafunzi ambao wanahitaji utulivu lakini tunalea vijana ambao wanaposikia haya mambo na kuyaona mara kwa mara wanaona ni jambo la kawaida wanatakiwa kulifanya.

Nakumbuka kuna wakati jijini Dodoma ilianzishwa operesheni ya kukamata wanaopiga muziki hadi usiku mnene. Cha ajabu kwa sasa wamerudi kama kawaida na wako wanaokesha hadi asubuhi kuanzia Ijumaa hadi Jumatatu.

Bila kuchukua hatua kwamba tumeamua kuondoa uchafu wa kelele tutaendelea kuwa na sehemu kubwa ya jamii ya mjini ya hovyo na kuendelea kuharibu watoto.

Lazima kuwe na usimamizi thabiti wa kumbi za starehe ni kweli nchi inataka kodi na tunataka kuona biashara zinastawi ili kurahisisha maisha ya watu, lakini ustawi wa watu kiafya na kiakili ni muhimu mno.

Kwa mfano katika jiji la Arusha kuna eneo linaitwa stress free zone huko ni balaa lingine, unakutana watoto wa umri wa kati wanajiuza kiasi cha kujiuliza ni kizazi cha aina gani cha baadaye kinaandaliwa.

Kote huko muziki ni usiku kucha kiasi cha kujiuliza mamlaka za serikali hazioni?, hatua gani zinachukuliwa kwanini kusiwe na utaratibu wa kutengeneza maeneo haya yasiwe kero kwa wengine?

Unapotembelea nchi zilizoendelea kama Marekani, Thailand na Denmark wanafanya starehe, wana kumbi nzuri za kisasa na huwezi kukuta inakuwa kero kwa wengine,utamaduni huo umejengwa na umezoeleka.

Tunaweza kusema huenda nchi hizo ni kwa sababu zina baridi muda mwingi, lakini kuna nchi kama Afrika Kusini na Botswana ni nadra kukuta kelele za kumbi za starehe, maana yake ni kiwango cha juu cha kustaarabika na usimamizi thabiti wa sheria unaofanywa na mamlaka husika.

Ni muhimu NEMC ikachukua hatua ili kukomesha tabia hizi,naamini wakichukuliwa hatua pasipo kuangalia vyeo au fedha walizonazo, bali kujali ustawi wa wengine na siyo kujali fedha hali itakuwa nzuri.

Kama ni eneo la starehe tupu kama Mlimani City ambako hakuna makazi ya watu karibu hiyo haina neno,lakini ikiwa ni jirani kabisa na watu ni kuwaumiza kwa makusudi na kuwanyima haki yao ya kikatiba.

# HARUSI









Familia ya Mwaimu ilikuwa na furaha baada ya kupata nafasi ya kumuaga binti yao, Hilda Mwaimu, kabla ya kufunga ndoa. Sherehe ilifanyika Mei 28, ukumbi wa Mbezi Guarden jijini Dar es Salaam.

MITINDO









## MALKIA ELIZABETH

# Mitindo mavazi yake hatari

MALKIA Elizabeth wa Uingereza ni mwanamke anayeongoza kwa kupigwa picha nyingi zaidi katika historia ya utawala wake wa miaka 70.

Hata hivyo, kinachowavutia watu wengi ni ubunifu wa hali ya juu wa mitindo ya magauni na makoti yake ya rangi zinazong'aa sambamba na kofia zinazofanana rangi na nguo.

Malkia huyo, anaingia katika orodha ya watu wanaopendeza zaidi wanapovaa nguo mbalimbali kwa mpangilio wa kushangaza.

Ukiachana na aina ya mavazi yake, mkoba wake maarufu wenye umbo la mraba, akifuatiwa na kidani cha lulu inamfanya kuwa na mwonekano wa kuvutia.

Uvaaji wa Malikia Elizabeth umekuwa ukiboreshwa zaidi katika miongo saba ya utawala wake, ukisaidiwa na uhusiano wa karibu alionao na wabunifu na wavaaji wanaoaminika.

### UBUNIFU WA MITINDO

Alipokuwa na umri wa miaka 20, Princess Elizabeth alianza kufanya kazi na mbunifu Norman Hartnell, ambaye alikuwa akimvalisha Mama ake.

Alipochukua kiti cha umalkia, Hartnell alimsaidia kumg'arisha katika hafla za serikali na ziara za kifalme akiwa amevalia gauni nyingi zilizobuniwa kwa vitambaa vya tulle na satini, zilizopambwa kwa mbegu za lulu, crystals na shanga.

Hartnell pia alimtengenezea nguo mbili muhimu zaidi ambazo ni- vazi lake la harusi na gauni alilovaa wakati wa kutawazwa kwake.

Kisha Ian Thomas alimchukua katika miaka ya 1970 na 1980 kwa mfululizo wa nguo za chiffon ya rangi ang'avu, zenye maua na pinde.

Kwa miaka 24 iliyopita mavazi yake yamebuniwa na kuzalishwa ndani ya nyumba na timu ndogo ya watu wapatao 10, wakiongozwa na mvalishaji wake binafsi wa nguo Angela Kelly.

UREMBO



JING'ARISHE KIPUPWE

# Ngozi ibaki laini wakati wote

MSIMU huu wa kipupwe, changamoto kubwa ni uwepo wa upepo unaoambatana na baridi kali.

Hali hii kwa wengine inawaathiri kwa kukakamaa kwa ngozi, kukatika midomo na miguu.

Hata hivyo, unaweza kufanya mambo kadhaa yatakayosaidia kuitunza ngozi yako.

**Kunywa maji ya kutosha**

Wakati huu aghalabu watu wengi hawana mazoea ya kunywa maji sana katika hali ya kijibaridi, lakini njia yenye matokeo mazuri ni kujitahidi kunywa maji ya kutosha.

Kwenye maji yako pia unaweza kuongeza limau au ununue maji yenye ladha tofauti.

**Ongezea Face oil kwenye mafuta yako**

Ukimaliza tu kupaka moisturiser yako, jipake face oil ili kutunza unyevu unyevu na hautahisi ukavu zaidi.

**Usiskrab uso zaidi ya mara moja**

Wakati wa kipupwe, ngozi inapoteza unyevu kwa urahisi. Ukishindwa kulainisha ngozi yako unaandaa mazingira mazuri ya ngozi kukauka na hautajisikia vizuri. Skrab' kwa sasa ufanye mara moja tu kwa wiki. Usizidishe kwa sababu utasababisha ukavu zaidi.

Na baada ya kumaliza kufanya scrub yako, tumia maski papo hapo uifanyie haki ngozi yako.

**Tumia hand creams**

Usiache mikono yako ikawa mikavu. Hakikisha unatumia hand cream.

**Weka mafuta kwenye midomo**


Kwenye midomo tumia mafuta ya balm na jelly, tena ikibidi uwe unaweza kuibeba kwenda nayo sehemu mbalimbali.

Kwa wewe ambaye una tabia wakati sehemu za mdomo zimekauka unalambisha mate wakati wa kipupwe na baridi kufanya hivi hakutakusaidia. Isitoshe, unaweza kupata vidonda.

**Nguo zakufunika mwili**

Hizi ni nguo ambazo wewe mvaaji utakuwa sawa unapofanya shughuli zako. Kumbuka unapojiacha wazi, upepo ukikupiga utakauka zaidi. Fanya chaguo bora la nguo unazovaa.





MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Jilambe kashata za maziwa ya unga

KASHATA ni kichangamsha mdomo ambacho mtu anaweza kula wakati wowote anapojisikia kutaka kujiburudisha kinywa chake.





**Mahitaji**

Maziwa ya unga kikombe kimoja na nusu, sukari kikombe kimoja na robo, maji kikombe kimoja na nusu na Arki ya vanilla kijiko kimoja cha kula.

Mahitaji rangi ya chakula kijiko kimoja cha kula (machungwa) na mafuta ya kupikia vijiko viwili vya kula.

**Namna ya kuandaa**

Tumia sufuria au pan tia maji na sukari na acha ichemke.

Ikianza kutoa mapovu mazito kuanzia dakika nane hadi 10, weka rangi , arki na mafuta ya kupikia, koroga kidogo na wacha ichemke tena.

Ukimaliza subiria tena kwa dakika tatu mpaka tano au iwe nzito ukiigusa kwa vidole viwili ukiachia ifanye kama uzi au mfano wa gundi.

Weka maziwa ya unga koroga haraka haraka kwa dakika moja au mpaka mchanganyiko uwe mzito.

Kisha paka mafuta sehemu yako ya kukatia au trey, weka mchanganyiko wako, tumia mwiko, kijiko au kifimbo kuwekea sawa, wacha upoe na ukate shape unayopenda na zitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Umuhimu wa vifaa bora katika ujenzi wa ukuta wa nyumba yako

UKUTA wa nyumba ni sehemu muhimu na ya kudumu na ndio hushikilia ustawi na uimara kwenye nyumba au jengo lolote.

Mara nyingine matokeo ya nyumba nzuri na uimara wake huonekana kwa nje ikiwa imenakshiwa vizuri bila kujua siri ya vitu gani vilivyotumika mpaka kufikia kuonekana katika hali hiyo.

Mtaalam wa ujenzi, Victor Mkalama, anasema ukuta anaozungumzia ni ule ambao hutokana na mchanganyiko wa zege au mawe na kufanyiwa utaalam wa uashi na kusimama kama ukuta ambao baadaye huitwa nyumba.

Anasema jambo la msingi la kufahamu katika kutambua kama unataka kuwa na ukuta wa nyumba bora, imara na wa kudumu ni kuhakikisha unakuwa makini na aina ya malighafi unayotumia ambayo yanaendana na mazingira ya eneo husika.

Jambo lingine, anasema la kuzingatia ni mtindo na muundo wa nyumba husika

"Na katika hili unapaswa kufahamu pia kwamba nyumba unayojenga ni ya mtindo na ya muundo gani na pia kama ni wa kutumia mawe au tofali ili fundi anayejenga akushauri kutoka na mazingira ya eneo lako," anasema Mkalama.



"Ukuta bora, imara na ambao ni wa kudumu unategemea sana na aina ya malighafi. Ikumbukwe kwamba ukuta wa tope, mawe au tofali ubora na uimara wake hutofautiana sana, na ndiyo maana tunashauri sana kupata ushauri kutoka kwa wataalam.

"Kwa hiyo hata katika ufundi katika kujenga nyumba yenye ukuta bora hakuwezi kutokana na ubunifu pekee kutoka kwa fundi, unategemeana sana na hivyo vitu vitatu ambavyo ni malighafi, mazingira ya eneo ambalo nyumba husika inajengwa na muundo wake, halafu ufundi ni wa mwisho," anasisitiza.

Pia anasema katika kazi ya kujenga ukuta wa nyumba au wa jengo lolote ni lazima kuzingatia uzito unaoendana na jengo husika.

"Ukuta usioendana na aina ya jengo unaweza kuleta shida kwenye jengo au nyumba baadae. Na aina ya kwanza ya ukuta unaobeba uzito wa jengo hujengwa kwa kutumia tofali za kuchoma, mawe au matofali ya zege au mchanga.

"Kazi ya ukuta wa aina hii hufanya kazi kubwa ya kuchukua na kusafirisha uzito wa paa au jengo hata kama ni nyumba ya kawaida au ghorofa," anamalizia.

## Jinsi ya kutumia Microwave kupikia vyakula



WENGI tumezoea kifaa cha Microwave hutumika kwa kupasha moto vyakula ndani ya dakika tano, tayari kwa kuliwa.

Kama chakula ni baridi huna haja kutumia muda mwingi kukipasha moto, lakini kwa kutumia chombo hiki ni muda mfupi tu, kinakuwa tayari.

Hata hivyo, kuna Microwave zina hadi dakika 30, ukitumia dakika 30 na 'Maximum heat'bila shaka unaweza kupika vingi.

Ili kufahamu zaidi namna ya kuitumia naomba tufahamu ni vyakula gani unaweza kupikia ama kwenye microwave?


**1.** Kuchoma viazi vitamu na ndizi mzuzu itakubali pia, jambo la msingi ukishaiandaa ichome chome na kisu, uma au pasua kidogo ili ipate hewa muda wa kuiva iive hadi ndani naweka dakika 10 medium na 10 high heat.

**2.** Mboga mboga unaweka dakika 10 medium heat

**3.** Samaki wekea viungo weka kwenye karatasi ngumu, kama hutaki asikauke sana usifunge na mfuniko.

**4:** Pia kwa kutumia muda kama huo unaweza kuoka pizza na keki.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO... ...KUMBE KUNA 'WALIMWENGU NA WALI'NAZI'...

# Mmoja auawa katika maandamano Sudan

**KHARTOOM,** SUDAN

MADAKTARI nchini Sudan wamesema mtu mmoja miongoni mwa waandamanaji ameuwawa kwa kupigwa risasi katika mji mkuu Khartoum juzi.

Kufuatia tukio hilo, mtaalamu wa haki za binadamu wa Umoja wa Mataifa, Adama Dieng, ameitaka mamlaka nchini humo kujizuia kutumia nguvu kupita kiasi dhidi ya waandamanaji. Maelfu ya raia waliingia barabarani mjini Khartoum na miji mingine, wakidai haki kwa watu waliouwawa wakati wa maandamano ya kudai demokrasia ya mwaka 2019 dhidi ya kiongozi aliyeondolewa madarakani Omar al-Bashir. Maandamano hayo yalifanyika wakati mtaalam huyo kuhusu haki za binadamu nchini Sudan alipotembelea kwa mara ya pili tangu kutokea kwa mapinduzi.

Siku ya Jumatano jeshi lilikutana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa,Umoja wa Afrika na Jumuiya ya ushirikiano wa maendeleo wa serikali za nchi za Upembe wa Afrika,IGAD na kukubaliana kuanzishwa kwa mazungumzo ya moja kwa moja kati ya makundi mbalimbali nchini humo, yatakayofanyika juma lijalo.

# UN yaongeza muda ukaguzi wa meli Libya

**NEWYORK,** MAREKANI

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa limeidhinisha azimio la kuongeza uidhinishaji kwa nchi na mashirika ya kikanda kukagua meli kwenye bahari kuu na pwani ya Libya.

Hatua hiyo inatokana na kushukiwa nchi hiyo kukiuka vikwazo vya silaha vilivyowekwa na Umoja huo.

Katika azimio hilo lililorefusha kipindi cha ukaguzi kwa mwaka mmoja mbele, Russia haikupiga kura.

Juhudi za usimamizi wa operesheni hiyo inayojulikana kama Irini neno linalomaanisha amani, zilianzishwa na ujumbe wa Umoja wa Ulaya tangu mwezi Machi 2020.

Umoja wa Ulaya ulisema jukumu la msingi litakuwa kutekeleza vikwazo vya silaha vilivyowekwa na Umoja wa Mataifa, kupitia anga, satelaiti na mali za baharini.

Balozi wa Russia katika Umoja wa Mataifa Vassily Nebenzia, alisema, alitaraji operesheni hiyo ingechangia kupunguza usafirishaji haramu wa silaha na kutumia juhudi za kisiasa katika kutuliza mzozo wa muda mrefu nchini humo.

**Habari zote DW na BBC**



Askari wa kulinda amani kutoka Senegal akiwa katika majukumu yake karibu na mji wa Timbuktu nchini Mali juzi baada ya wanajeshi wawili kufa kwa kulipukiwa na bomu la kutegwa ardhini. **PICHA: DW**

# UTATA WAZIDI UKRAINE

## Russia yadai kusonga mbele Donetsk Ukraine yakomboa baadhi ya maeneo

**KYIV,** UKRAINE

TAARIFA katika mstari wa mbele wa mapambano nchini Ukraine, zinaripoti vikosi vya Russia vinazidi kusonga mbele katika jaribio la kudhibiti jimbo la Donbas.

Juhudi kubwa zimeelekezwa maeneo ya Severodonetsk na Bakhmut yaliyoko mashariki mwa nchi hiyo

Hata hivyo mji wa Severodonetsk, unazidi kushambuliwa kwa makombora.

Katika hatua nyingine, vikosi vya Russia vilirudi nyuma baada ya kushindwa kwa majaribio ya kusonga mbele kuelekea katika mji wa Bakhmut, hadi kusini-magharibi katika mji wa Severodonetsk .

Katika jimbo la Donetsk ,Russia inapiga makombora katika ngome za wanajeshi wa Ukraine katika eneo lote kwa kutumia vifaru na ndege za kivita, lakini kasi ya kusonga mbele katika eneo hilo imepungua kwa sababu jeshi limekosa ari.

Ndani ya eneo la Lyman, Warussia wanajaribu kuchukua udhibiti wa ukanda wa kushoto wa mto Seversky Donets ili kuzuia misaada kuingia.

Ndege ya kijeshi ya Ukraine yadunguliwa

Russia imesema vikosi vyake vimedungua ndege ya kijeshi ya Ukraine iliyokuwa inasafirisha silaha na zana za kivita karibu na bandari ya Bahari nyekundu ya Odesa.

Wizara ya Ulinzi ya nchi hiyo, ilisema jana katika taarifa yake kuwa ndege hiyo ilikuwa ikisafirisha silaha na zana za kivita.

Ilisema pia kwamba shambulio la kombora walilolifanya lilipiga eneo ambalo ni kituo cha mamluki wa kigeni. Awali maofisa wa Ukraine walidai kuwa kiwanda cha kilimo kimepigwa na kombora hilo katika eneo la bandari ya Odesa.

Hata hivyo, Wizara hiyo ilisema makombora yalipiga kituo cha mafunzo ya makombora katika jimbo la Sumy nchini Ukraine ambako waalimu wa kigeni walikuwa wakitoa mafunzo kwa vikosi vya Ukraine.

Ukraine yarejesha mji wa viwanda

Wakati huo huo, Ukraine imesema imerejesha tena udhibiti wa sehemu ya mji wa viwanda wa Sievierodonetsk.

Eneo hilo ndiyo shabaha ya mashambulizi ya vikosi vya Russia katika mkoa wa mashariki wa Donbas, na inaweza kulishikilia kwa hadi wiki mbili wakati mapigano yakiendelea.

Gavana wa jimbo la Luhansk, Sergiy Gaidai, alisema wapiganaji wa Ukraine wamechukua asilimia 20 ya eneo ambalo walilipoteza huko Sievierodonetsk.

Vikosi vya Russia vimetumia mizinga kufanya operesheni za mashambuilizi katika jiji hilo.

Kwa mujibu wa jeshi la Ukraine vikosi vya Russia vimerudi nyuma baada ya mashambulizi kadhaa kushindwa katika mji wa jirani wa Bakhmut na kutolifikia eneo la Sievierodonetsk.

Katibu Mkuu wa NATO azungumza na Erdogan

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Kujihami (NATO), Jens Stoltenberg, amezungumza na Waziri Mkuu wa Finland na Rais wa Uturuki kujaribu kuondoa upinzani kuhusu nchi hiyo kujiunga na jumuiya hiyo.

Finland na Sweden zilituma maombi ya kujiunga na muungano huo wa kijeshi hivi karibuni.

Stoltenberg, ambaye alifanya ziara nchini Marekani wiki hii, alisema alikutana na Waziri Mkuu wa Finland, Sanna Marin, na walijadili haja ya kushughulikia wasiwasi wa Uturuki ili kusonga mbele kwa maombi yao ya uanachama wa nchi hizo mbili. Vita vya Russia nchini Ukraine vimeyasukuma mataifa hayo kuomba kujiunga na NATO, lakini rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan anazishutumu nchi hizo kuwa zinawaunga mkono wapiganaji wa Kikurdi wanaochukuliwa na nchi yake kuwa magaidi.

Stoltenberg alisema alikuwa na mazungumzo ya tija na rais Erdogan, akiitaja Uturuki kuwa mshirika muhimu, na kusifu juhudi zake za kuratibu makubaliano ya kuhakikisha usafirishaji salama wa nafaka kutoka Ukraine.

MAKALA

# SABABU ZA KUTOKUWA NA CHA KUWARITHISHA WATOTO WETU



Na Magabilo Masambu - 0689157789

MAANDIKO Matakatifu yanasema usimwache elimu aende zake. Ndivyo wengi wetu tunavyoamini kwamba ili mtu afanikiwe katika maisha yake ya baadaye, ni sharti apate elimu ya kutosha na kwamba huo ndio urithi pekee mzazi anaoweza kumwachia mtoto wake.

Jambo pekee tunalosahau ni kwamba pamoja na umuhimu huo wa elimu, ni kweli kwamba si kila aliyefanikiwa amepata elimu ya kutosha. Hata waliopata elimu hiyo ya kutosha kwa kiasi kikubwa, wanawategemea ambao hawakupata elimu ambao waliwekeza nguvu na akili zao katika shughuli ambazo hazihusiani na elimu.

Sina maana kwamba elimu haina maana lakini kuendelea kuamini kwamba ili ujitegemee ni kusoma peke yake ndiko kunafanya mtu anaanza darasa la kwanza mpaka anamaliza chuo kikuu huku hajawahi kujishughulisha na kitu chochote hata kibarua cha zege kwa sababu alishaaminishwa kwamba akisoma tu atakuwa na maisha mazuri. Kwa maneno mengine ni kama tunakuwa na kifungo katika kuwaza kupata shughuli nyingine nje ya elimu yetu. Hivyo sababu moja inayofanya tusipate cha kuwarithisha watoto wetu ni hiyo, kuwaaminisha kwamba urithi pekee ni elimu.

Sababu ya pili ambayo ni kubwa ni kudharau kazi tunazozifanya. Ukisikiliza karibu kila mtu hapendi kazi anayoifanya japo inamwingizia kipato ambacho kinamwezesha kuishi na familia yake. Ni watu wachache sana hasa Afika pengine zaidi Tanzania wanaopenda kazi wanazozifanya wazirithi watoto wao. Hii ni kwa sababu hakuna kazi duniani isiyokuwa na changamoto zake. Pia changamoto hizo kwa sababu zinatofautiana na za kazi nyingine huwa tunadhani kwamba wengine wana nafuu zaidi kuliko sisi.

Mtu anafanya kazi fulani lakini anawaambia watoto wake “Wanangu someni zaidi kwa sababu staki mje mfanye kazi kama yangu.” Anadharau kazi inayowasomesha watoto wake, inayomlisha na kumpatia mahitaji mengine maana yake kazi kama hiyo hataweza kuirithisha kwa watoto wake badala yake watoto pia wataanza upya katika kazi ambazo hawakuwahi kuziona kwa sababu wanayoiona baba kesha waambia ni mbaya.

Sababu ya pili ni kukosa kumbukumbu sahihi za kazi tunazozifanya ili kuwafanya watoto wetu wazifanye kwa bidii zaidi. Unakuta mtu ni mfanyabiashara, biashara zake hawahusishi watoto, hawaambii namna biashara zinavyokwenda, hawaonyeshi wateja wakubwa wa biashara zake. Hawaambii namna anavyopata faida na kukabiliana na changamoto za kupata hasara bali anawaambia watoto wake someni sana kwa sababu huo ndio urithi pekee nitakaowaachia, msijihusishe na biashara msije mkawa kama mimi. Siku anafariki dunia na biashara zote zinakufa kwa sababu hakuna hata mmoja anajua alivyokuwa anafanya biashara hizo.

Mtu ni polisi ameshakaa kwenye kazi hiyo muda mrefu, anashindwa kuwajengea baadhi ya watoto wake mazingira ya wao waje kuwa polisi wenye vyeo vikubwa zaidi kuliko yeye. Anawaambia hii kazi ina matatizo sana msije kuwa kama baba yenu someni sana msiwe polisi. Kumbe angekuwa anawahamasisha kwamba pamoja na kusoma mnaweza kuwa polisi wazuri zaidi kuliko mimi. Kadhalika na shughuli zingine pia tungelifanya hivyo hivyo.

Moja ya njia za kuwafundisha watoto wako kazi unazozifanya ni kuweka kumbukumbu ya kazi zako vizuri. Simaanishi kwamba watoto wako wote lazima warithi kazi unazofanya lakini kama kazi unayofanya inawalisha, inawavalisha, inawasomesha kwa nini hutaki wasiifanye kwa kiwango cha juu zaidi?

Juzi juzi nimesoma mahali fulani kuhusu hadithi ya binti mmoja mdogo mwenye umri wa miaka 19 kwa jina anaitwa Zara Rutherford, raia wa Uingereza na Ubelgiji ambaye amekuwa rubani mdogo kabisa kuruka na kuzunguka dunia na ndege. Nilipofuatilia niligundua kumbe hata wazazi wake ni marubani. Maana yake ni kwamba kazi hiyo amejifunza kutoka nyumbani kwenda shuleni lakini sisi wa kwetu hatutaki wafanye kazi tunazozifanya tena tunawaambia ni hatari sana. Mbona wewe unazifanya na hujafa?

Binafsi naweza kusema mimi ni matokeo ya haya ninayoyazungumza. Nilianza kufahamu kuwa mimi ni mwandishi mwaka 2014 pale kazi yangu ya kwanza ilipotoka kwenye magazeti. Sikufundishwa na mtu kuwa mwandishi lakini nilichoshangaa ni kwamba siku moja nikiwa na albamu ya picha za marehemu baba yangu wakati nikizipanga vizuri nikakutana na vipande vya magazeti vya gazeti la Majira ambavyo vilikuwa na makala za baba yangu alizokuwa anaandika miaka ya 1990 akiwa amevipachika nyuma ya picha.

Pamoja na kwamba hakuwahi kuniambia kuwa amewahi kuwa mwandishi wa makala, vipande hivyo vya magazeti vilinitia moyo na hamasa ya kufanya kazi ya uandishi kuwa sehemu ya maisha yangu.

Jambo pekee nililokuwa naliona nikiwa mdogo ni kuona baba yangu akipenda sana kununua magazeti na vitabu. Kwa hiyo kuna haja ya kuweka shughuli zetu wazi ili kuwahamasisha watoto wetu wazifanye kwa kiwango cha juu kabisa kuliko sisi tutakakoishia. Tusione urithi pekee ni elimu tufikiri upya kuzihusu kazi zingine hasa tunazozifanya tukizingatia kwamba kwa sasa kila mtu ni msomi, hivyo watu wote hawatakuwa mameneja ofisini.

Kama ni mkulima, fundisha watoto wako kilimo kwa sababu watakuwa na elimu kuliko wewe, watalima kisasa zaidi. Kama ni fundi ujenzi, fundisha watoto ujenzi kabla ya kwenda chuo kikuu ili wawe na hamasa ya kusoma uhandisi kutokea nyumbani kwenda shuleni na kadhalika.

Tusidharau kazi tunazozifanya kwa sababu hakuna kazi nzuri kwa anayeifanya bali ni kazi nzuri kwa asiyeifanya. Ukiwa mkulima unaona profesa wa chuo kikuu anafaidi kwa sababu hujajua kwamba halali kwa kazi nyingi alizo nazo. Ukiwa mwalimu unatamani kuwa daktari wakati hata kumng'oa mtoto wako jino unaogopa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Wanamuziki zamani walivyofunda changamoto kwenye mapenzi, ndoa*



Na Adam Fungamwango

WAKATI kizazi cha sasa kinaendelea kula ngoma za mapenzi kila kukicha ‘nakupenda nakupenda’ kiasi kwamba wasikilizaji wake ambao ni vijana hudhani huwa hakuna changamoto yoyote ile. Hebu leo tukumbuke wanamuziki wa dansi walivyokuwa wakiyazungumzia mapenzi kwa namna tofauti.

Mapenzi haya haya ambayo wasanii wa sasa kila siku wanatoa nyimbo kama vile siku zote mapenzi yako poa tu, wale wa zamani walieleza changamoto nyingi kwenye ndoa na mepenzi. Kwa hiyo wasikilizaji na mashabiki wa muziki walijifunza vitu vingi kuwa ndoa ina mabonde na milima, ina tamu na chungu.

Walifundishwa kuwa ndoa au mapenzi hayana raha kwa asilimia 100 bali kuna sehemu kunakuwa na changamoto ambazo wanabidi wapenzi au wanandoa kuzikabili.

Walieleza kuwa mapenzi au ndoa ni kitu muhimu kwenye jamii na kila binadamu anatakiwa kuwa nacho, lakini pia kwenye baadhi ya nyimbo wanatoa angalizo au kufundisha jinsi mapenzi au ndoa zinavypoingia mizozo na jinsi ya kukabliana navyo.

Kwa sasa tumeanza kusikia watu wanauana, wanapigana, wanafanyiana mambo ya ukatili kwenye ndoa au mapenzi, nadhani kwa sababu ya kuaminishwa tu kuwa ukiingia kwenye mapenzi, basi wewe ni raha tu.

Nyimbo za kisasa wala hata haziwakumbushi kuwa wanaoingia kwenye mapenzi au kuoana inabidi wavumiliane kwa shida na raha kwa sababu kuna mmoja anaweza kuugua, mwenzake anatakiwa kufanya kazi ya kumuuguza kwa sababu huo ndiyo upendo wenyewe. Si mmoja anaumwa, mwingine anamtelekeza, au kuchukua kilicho chake na kuondoka.

Kwa haya yanayotokea kwenye ndoa au mapenzi kwa sasa, wasanii wa bongo fleva wana kazi ya kuelimisha ili tusisikie tena watu wakitwangana risasi, au kuuana na kufukiana shambani, kufyekana na mapanga au hata kufyekana uume.

Tuanze na ‘Ndoa ya Mateso’ wa Hayati Majirani Rajabu. Ni wimbo ambao mama yuko kwa mjumbe wa nyumba kumi anamwelezea matatizo ya mumewe. Anamshangaa mumewe kamtoa nyumbani kwao kwa vigelegele na heshima nyingi, lakini sasa amemgeuka.

Mume hashikiki, kazi yake ni ulevi na watoto hawajali. Mke akaomba ushauri kwa mjumbe. Mjumbe anamwambia avumilie kidogo kwa sababu wameshazaa watoto, kwa hiyo watamwita wamkanye. Akirudia, basi mjumbe atakuwa shahidi kwa kitakachotokea. Na wala hatokuwa na maneno tena mke akitaka talaka yake au kwenda kwao.

Hapa tunaona jinsi wimbo huo unavyofundisha kuwa na subira, pamoja na kwenda kuongelea matatizo sehemu husika na si kwenda kuwaambia marafiki au mashoga, ambao wengine wanakuwa ni wachonganishi tu. Kama msikilizaji hakuelimishwa hivi, basi ungeweza kusikia kaua mwenzake, au yeye mwenyewe kajiua.

‘Jiko Limenuna’ ni wimbo uliopigwa na Vijana Jazz, ukimzungumzia mama mmoja ambaye alikwenda kumueleza shemeji yake kuhusu matatizo yalivyo katika ndoa yake.

Pamoja na kwamba mumewe amekuwa halali nyumbani, anacholalamika zaidi mke ni kutoachiwa hata pesa za matumizi kiasi cha kushinda na kulala na njaa. Mke anasema angekuwa peke yake angejinyonga, lakini moyo wake wote ni kwa watoto.

Wanamuziki wanafundisha hapo kuwa hata kama mke akijinyonga kukimbia matatizo, watoto atawaacha duniani nao wataishije? Hapa inamfikirisha hata mtu ambaye ana wazo la kufanya hivyo. Hiyo ndiyo elimu ya muziki wa zamani.

‘Ilikuwa lifti tu’ ni wimbo mwingine wa Vijana Jazz, ambao mume anamtuhumu mke juu ya uaminifu wake. Anashindwa kumwelewa baada ya kumpa kijana lifti kwenye gari, lakini ni kama wanafahamiana hivi kwa tabasamu na vicheko vilivyokuwa ndani ya gari kiasi cha kumfanya achanganyikiwe.

Mke anamjibu mumewe kuwa yule ni kijana tu wa kawaida, kwani alipotoka nyumbani Oysterbay kufika Salender gari lilizimika, yule kijana alimsaidia kusukuma na kumpa lifti tu, hivyo asiwe na wasiwasi.

Hii inaonyesha kuwa mambo haya ya wasiwasi, wivu, vingine vinavyofanana na hivyo kwenye ndoa na mapenzi vilikuwapo tangu enzi hizo na vitaendelea kuwapo na havikwepeki. Hebu angalia hapo, lifti tu, jamaa kaanza ‘kumaindi’.

“Nenda Ukaishi Salama’ ulikuwa wimbo wa UDA Jazz, unamzungumzia jamaa aliyetorokwa na mpenzi wake, akaenda kuishi na rafiki yake. Ukweli ni kwamba inauma sana. Unaweza kuua au kujiua. Lakini kwenye wimbo huu, mtunzi anamwambia mpenzi wake nenda ukaishi salama, pamoja na kuyafanya haya na rafiki yangu, nakutakia maisha mema uendako.

Ni kwamba chochote kitakachokupata duniani, kama hakijakuondoa uhai wako, basi maisha ni lazima yaendelee. Unaweza kupata mume, mke au mpenzi mwingine mbele ya safari ukasahau yote na kuona kama ulichelewa, ukaanza kujilaumu kuwa hivi kwa nini nilitaka kumdhuru mtu au kujidhuru mwenyewe.

Wanamuziki na wasanii wa sasa wana wajibu wa kutunga nyimbo za kuiambia jamii yetu kuwa mapenzi si raha tu moja kwa moja hadi mwisho. Mapenzi au ndoa yana tamu na chungu. Wanapooana watafanya sherehe kubwa, lakini maisha ya ndoa yana tabu na raha. Uvumilivu ni muhimu, hakuna mapenzi au ndoa inayokosa misukosuko.

Uvumilivu ni alama ya ushujaa katika mapenzi au ndoa, kwani ngome ya mapenzi haivunjwi na fitina, au mawimbi yanapowapiga wapenzi wakiwa kwenye safari yao.

**Tuma meseji 0714 350534**

# HADITHI

PRINCE Petit kijana aliyelelewa kwenye mazingira ya ajabu. Amelelewa na baba yake mzazi tu bila mama. Madada wa kazi waliopewa kazi ya kumlea walipewa mkataba wa mwaka mmoja mmoja tu na wanapomaliza hawakuongezwa. Hakupelekwa shule yoyote ile, badala yake walimu walilipwa pesa kwa ajili ya kumfundisha nyumbani tu. Hata alipokuwa akipata nafasi ya kwenda kufurahia maisha na kuitazama dunia nje ya nyumba yao, alipewa angalizo la kutozoena na mtu yeyote yule. Aliingiziwa falsafa na vitu vingine kichwani mwake mpaka akawa na tabia ambazo ni tofauti na umri wake. Akiwa na miaka mitano tu, alianza kufundishwa kulenga shabaha na alipofikia miaka minane tu alikuwa na uwezo wa kutumia bastola ya aina yoyote ile na angeweza kuajiriwa kwenye shirika lolote la kijasusi duniani Anapofika umri wa miaka 25, baba yake mzee Pokwa anamtuma kazi. Kazi ya kuua na kulipiza kisasi. Ni kwa nini? Anakwenda kumuua nani? Kwa nini baba anayejua mkasa mzima asiende mwenyewe? Kitu gani kilichotokea huko nyuma? Nakala yako ya Nipashe itakufanya kujua kilichopo nyuma ya pazia.

# Mwisho wa Mauaji-4

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

WOTE walikaa kimya kwa muda wa dakika nzima hivi. Kila mmoja alikuwa anatafakari.

"Baada ya hapo shamba likachukuliwa?" Prince akauliza.

"Ndiyo. Walichukua shamba la babu na bibi yako, ambalo mama yako ilikuwa alirithi. Ni kwa sababu wakati wanamuua mama yako, yule aliyefungua mlango wa gari na kumpiga risasi, alichukua na zile nyaraka halisi na kutokomea nazo kusikojulikana."

"Wapo hao watu hadi leo hii?"

"Umesahau mwanangu, ndiyo hawa ambao umeshaanza kuwamaliza. Umeanza na mmoja. Bado wengine."

"Sawa baba, lakini hujaniambia mimi nilikuwa na umri gani wakati mama anauawa?"

"Ulikuwa na miaka miwili. Niliumia sana. Kupoteza mke ambaye alikuwa mjamzito, na wewe ulikuwa bado mdogo."


"Sasa baba, kwa nini ulinilea kwenye mazingira haya?" Yalikuwa ni maswali mazito aliyoulizwa mzee Pokwa na kijana wake, ambayo hakuwahi kuulizwa kabla.

"Waliochukua roho ya mama yako walikuwa wanataka pia waihitaji roho yako."

Prince alishtuka.

"Ndiyo mwanangu, walijua ukikua na kusimuliwa kisa hiki ungelipiza kisasi. Hawakuwa na shida na mimi. Walijua nitalia, nitaugulia, lakini baadaye naweza kupata mke mwingine nikamuoa. Wewe huwezi kupata mama mwingine. Walitaka kumaliza kizazi cha mama yako, ambaye ni wewe tu mmoja. Ulionekana unaweza kuwa si hatari kwao, lakini hata kizazi chao. Kama usingewakuta hai wao, basi ungeweza kudili na watoto wao au wajukuu." Pokwa aliongea kwa sauti ya masikitiko, huku Prince akisisimkwa kutokana na habari hiyo.

Hapo ndipo alipojua ni kwa nini baba yake alifanya yote hayo.




**"Ahsante baba kwa kunifunulia yaliyojificha. Umekaa na kidonda hiki kwa muda mrefu. Leo umeamua kunifunulia nikione. Nakuahidi sitokuangusha. Nitawamaliza wote waliomuua mama yangu mzazi. Alikuwa anaitwa nani?"**

"Nilikulea kwenye nyumba hii ni usiri na uficho mkubwa ili usijulikane uliko. Ulitafutwa usiku na mchana ili uuawe. Walijua kama mama yako alianza kupigania mali za wazazi wake, isingekuwa kazi kubwa wewe pia kupigana kulipa kisasi cha babu, bibi kwa mali zao kuchukuliwa kirahisi, pamoja na dhuluma , pamoja na kuuondoa uhai wake."

Prince alikunja sura kwa hasira. Pokwa alimtazama kijana wake na kutabasamu.

"Nauliza swali la mwisho."

"Uliza mwanangu." Tabasamu la mzee Pokwa lilikoma ghafla.

"Kwa nini wewe hukuifanya kazi ya kulipa kisasi cha kuuawa mama?"

Baba alimtazama kijana wake kwa mshangao kidogo, baadaye tabasamu jepesi likachukua nafasi yake.

"Hili ni swali zuri zaidi kuliko yote ambalo umeniuliza." Akasema kwa sauti nzito.

"Ni kwamba nina uwezo hata leo wa kuwafagia wote waliokufanyia hivi, au waliotufanyia haya, lakini hivi fikiria mwanangu, ningelipa kisasi wakati wewe ungekuwa mkubwa na kukusimulia haya, wakati mwingine usingeweza kuamini kitu kama hiki.

Nilitaka uamini wakati unawaona maadui walioungana kumdhulumu mama yako mali ya wazazi wake na kumuua. Kwa bahati nzuri wote wapo. Nilitaka ujue kitu kama hiki, nikusimulie na maadui wawepo ili uamini. Ushahidi pekee ambao ungeweza kukubali ni kuwepo kwao. Hata kama wengine wakiwa wamefariki, lakini wengine wangekuwepo. Kwa bahati wote wapo."

Alishusha pumzi na kuendelea kuongea huku akimtazama kwa makini kijana wake.

"Kingine, nilikuwa nataka wewe ndiwe ulipe kisasi. Ndiyo maana nimekujenga kwenye mazingira hadi tangu mdogo. Ningekuacha na kuishi kama watoto wengine, saa hizi ungekuwa huwezi hata kuchinja kuku. Ungekuwa unaogopa. Nimekulea katika mazingira haya, si kwa ajili ya kukuficha na waliokuwa wanataka roho yako peke yake, lakini kukufundisha ukakamavu na ujasiri.

Yote hii ili siku nikikuambia jambo kama hili isiwe ni kulialia tu, bali ni kufanya kazi ambayo nitakutuma. Ndiyo maana leo hii unaweza kutumia bastola vizuri sana. Nimekufundisha ukiwa mdogo kwa ajili ya kazi hii. Na kwa bahati nzuri inaonekana unaiweza. Na tayari umeianza." Akamaliza na kuendelea kumuangalia Prince huku akitabasamu.

Ilikuwa ni tofauti kwa Prince, yeye alikuwa amekunja sura. Yote aliyozungumza baba yake yalikuwa yamemwingia kichwani.

Ndipo alipogundua kuwa yote yale ambayo alikuwa akifanyiwa akiwa mdogo. Kuishi kwa kufichwafichwa, kufundishwa ujasiri, kutojichanganya na watu, ukakamavu pamoja na kufundishwa jinsi ya kutumia silaha, ilikuwa kuimarishwa ili kulipiza kisasi.

"Ahsante baba kwa kunifunulia yaliyojificha. Umekaa na kidonda hiki kwa muda mrefu. Leo umeamua kunifunulia nikione. Nakuahidi sitokuangusha. Nitawamaliza wote waliomuua mama yangu mzazi. Alikuwa anaitwa nani?"

"Jina lake kamili lipo nyuma ya hiyo picha." Alijibu mzee Pokwa na kumpa mkono kijana wake.

"Umekua sasa mwanangu. Wakati naanza mkakati huu sikutegemea kama utafanikiwa. Nilidhani utakuwa mtoto goigoi. Ndiyo maana nilitumia nguvu sana kukuandaa. Kuna wakati nilijua nitashindwa, lakini sasa najivunia nimepata mtoto jasiri."

"Anayefuata ni nani?" Prince akauliza kwa hasira.

"Tulia kwanza kijana wangu, usiwe na hasira sana. Kazi hii haihitaji hasira. Ukiwa na hasira utaharibu. Hutoweza kufanya kazi kwa ufanisi."

Alipomaliza kuongea maneno hayo, aliinuka na kwenda kwenye kabati kubwa. Aliporejea alikuwa na picha ya mtu mwingine. Akamkabidhi kijana wake kama kawaida.

"Huyo anaitwa mzee Hassan. Huyu miaka mingi iliyopita wakati mama yako yu hai alikuwa kijana sana. Huyu ana hoteli yake kubwa pale Manzese Argentina. Huwa anafika pale kuanzia saa tatu usiku kukusanya pesa za mauzo ya siku. Inaitwa Upendo Hotel, iko kwenye kona tu ya barabara ya kwenda Tandale na ile kubwa ya Morogoro, wala huwezi kuipotea." Mzee Pokwa alitoa maagizo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# Poshy Queen kuachika ni ajabu?

MREMBO Poshy Queen, ambaye umbo lake linawatoa mate wanaume, amesema kuvunjika ndoa yake inatokana na changamoto za uhusiano.

Poshy ameachana na mumewe na baba mtoto wake, ambaye ni raia wa Nigeria na kusababisha wanaume kuanza kuwa karibu.

"Kwenye uhusiano huwezi kwenda sawa kila siku, sisi hatukuwa kwenye mapenzi kwa muda mrefu kwa sababu tulioana mapema, labda hatukujuana hatukukaa pamoja na vitu vingine vya kawaida," amesema.

## Q Chief amemganda Ali Kiba

MWANAMUZIKI mkongwe Q Chief, amemtaja msanii Alikiba kama chaguo lake la kwanza kutokana na tabia yake ya kutojikweza.

Amesema Ali Kiba yupo tofauti na mastaa wengine, hana mambo mengi na badala yake anaacha muziki wake uongee.

"Hana makeke, hana mambo mengi, ameacha mziki wake uzungumze kuliko mambo mengine na ndio maana namheshimu kila mara kutoka moyoni mwangu, " amesema.



## Moni kumbe unaogopa ufukara

RAPA kutoka Majengo Sokoni, Moni Centrozone, amesema bila kuwa na fedha kila mtu atakudharau.

Akizungumza na mashabiki wake kupitia Instagram, amesema kuna kipindi alitaka kupotea kutokana na makelele ya mashabiki wake ambao walimwona kama hajiwezi.

"Kuna kipindi watu wa Instagram walitaka kunitoa roho kwa mawazo, kama unavyojua hapa jijini usipojitetea kwa kipaji na kuonyesha uwezo wako hakuna wa kukusaidia," amesema.



## ZISIKUPITE

### RAPHINHA NA BARCA

KLABU ya Leeds United itapokea ofa ya pauni milioni 60 ili kumuuza nyota wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, ambaye amekuwa akihusishwa na kuhamia Barcelona. ***(The Athletic)***

### MANE KUAMUA

FOWADI wa Liverpool, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, ataamua kile waananchi wanachokitaka kuhusu mustakabali wake wa kubakia pale Anfield. ***(Sky Sports)***

### KANE KUSAINI

FOWADI wa Tottenham Hotspur na nahodha wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 28, sasa anaweza kusaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Express, via GiveMeSport)***

### WAN-BISSAKA KUUZWA

MLINZI wa Manchester United, Aaron Wan-Bissaka 24 anaweza kuuzwa kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### LUKAKU NA MSHAHARA

FOWADI wa Chelsea, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, yupo tayari kupunguziwa mshahara ili arudi Inter Milan, ambako aliondoka miezi 10 iliyopita kujiunga Blues hao kwa ada iliyoweka rekodi ya pauni milioni 97.5. ***(Telegraph)***

### BERGWIJN ATAKIWA

WINGA Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24 anatakiwa na Ajax, ambao wapo tayari kumpa mkataba mrefu hadi mwaka 2027. ***(De Telegraaf)***

### GVARDIOL AGOMBEWA

KLABU ya Tottenham Hotspur na Chelsea zinashindana kuwania saini ya mlinzi wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### ORIGI SAFI MILAN

AC Milan inatarajia kutangaza kumsajili fowadi wa Ubelgiji, Divock Origi mwenye umri wa miaka 27, ambaye ameshawaaga wachezaji wenzake wa Liverpool Liverpool. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### OLSEN KUBAKI VILLA

ASTON Villa wanakamilisha usajili wa pauni milioni 2.8 wa kumsajili golikipa wa AS Roma na Sweden, Robin Olsen mwenye umri wa miaka 32, baada ya kucheza kwa mkopo msimu ulioisha. ***(Mail)***

### TOLISSO KUONDOKA

KIUNGO wa Bayern Munich na Ufaransa, Corentin Tolisso mwenye umri wa miaka 27, anaweza kuhamia Ligi Kuu ya England wakati mkataba wake utakapomalizika Juni hii. ***(ESPN)***

### CHIELLINI HUYO MAREKANI

MLINZI mkongwe wa Juventus na Italia, Giorgio Chiellini mwenye umri wa miaka 37 anatarajia kuhamia Marekani katika Klabu ya Los Angeles FC. ***(Sky Sports Italia)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MANE: NITALAZIMIKA KUONDOKA LIVERPOOL

**Asema atafuata matakwa ya raia wa Senegal ambao wamepiga kura kumtaka atimke klabuni...**

**DAKAR,** Senegal

SADIO Mane atafuata matakwa ya watu wa Senegal linapokuja suala la kufanya uamuzi juu ya mustakabali wake pale Liverpool.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alihusishwa na kuhamia Bayern Munich siku chache kabla ya Liverpool kufungwa 1-0 na Real Madrid katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wiki iliyopita.**

Mane, ambaye amebakiza miezi 12 katika mkataba wake wa sasa pale Anfield, aliweka wazi kuhusu mustakabali wake baada ya pambano hilo lililofanyika kwenye Uwanja wa Stade de St Denis nchini Ufaransa.

Akizungumza na waandishi wa habari Ijumaa akiwa kwenye majukumu ya timu ya taifa ya Senegal, Mane alitoa dalili zaidi kwamba, mustakabali wake uko mbali na klabu hiyo ya Ligi Kuu England.

Alipoulizwa kuhusu kura ya maoni iliyoendeshwa na gazeti moja la nchini Senegal ambapo watu wengi walitaka aondoke Liverpool, Mane alijibu: "Niko kwenye mitandao ya kijamii na ninaona maoni yao.

"Si asilimia 60 hadi 70 ya Wasenegal wanataka niondoke Liverpool? Nitafanya wanavyotaka. Tutaona hivi karibuni.

"Msiwe na haraka maana tutaliona hili pamoja. Yajayo yatatueleza."

Mane aliichezea Liverpool mechi 51 katika msimu wa 2021-22 - ni wachezaji 10 pekee katika ligi tano kuu za Ulaya waliocheza zaidi yake - akifunga mabao 23 na kusaidia mengine mawili.

Amefunga mabao 90 ya Ligi Kuu England akiwa na Liverpool tangu alipocheza kwa mara ya kwanza Agosti 2016, ni Jamie Vardy pekee (104), Mohamed Salah (118) na Harry Kane (134) ndio waliomzidi kwa mabao.

Mchezaji huyo wa zamani wa Southampton pia aliiwakilisha Senegal katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika mapema mwaka huu na akafunga penalti iliyofanikisha kulibeba kombe hilo mbele ya Misri kwenye fainali.

Senegal, ambao waliwashinda wapinzani wao hao katika mechi ya mchujo ya kuwania kufuzu kwa Kombe la Dunia, Machi mwaka huu, jana Jumamosi walikuwa uwanjani kucheza na Benin kwenye michuano ya kufuzu AFCON.


SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
PORTUGAL
VERSUS
SWITZERLAND
1 | 1.72
X | 3.58
2 | 4.74

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+ GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCELONA, BAYERN ZAMUWANIA LUKAKU



**LONDON,** England

BARCELONA na Bayern Munich zimefahamishwa kuhusu mustakabali wa Romelu Lukaku na Chelsea wako tayari kumuuza mshambuliaji huyo, kwa mujibu wa 90min.

Lukaku alirejea Stamford Bridge msimu wa joto wa 2021 kwa uhamisho wa pauni milioni 97.5 kutoka Inter Milan, lakini amekabiliwa na wakati mgumu pale London Magharibi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alimaliza msimu akiwa na mabao nane pekee ya Ligi Kuu ya England katika mechi 26, akiachwa nyuma na Kai Havertz.

Pia alichunguzwa kwa kufanya mahojiano na vyombo vya habari vya Italia katikati ya msimu ambapo alitangaza nia yake ya kutaka kurejea Inter siku moja.

Kwa mujibu wa 90min, hapo awali iliripoti kwamba Chelsea haitamzuia Lukaku iwapo ofa inayofaa kutoka kwa Inter itawasili msimu huu wa joto, lakini sasa inaeleweka kuwa vigogo wengine wa Ulaya wanafuatilia hali yake pia.

Miamba ya Hispania, Barcelona na mabingwa wa Ujerumani, Bayern wamefahamishwa kikamilifu kuhusu mustakabali wake.

Hata hivyo, Lukaku anapendelea kurejea Inter, ambako aliisaidia kumaliza ukame wa kusubiri miaka 11 kutwaa ubingwa wa Italia, Serie A.



## Lacazette anaondoka Arsenal

**LONDON,** England

MSHAMBULIAJI wa Ufaransa, Alexandre Lacazette ataondoka Arsenal mkataba wake utakapokamilika Juni 30 mwaka huu, klabu hiyo imethibitisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 alijiunga na Washikabunduki hao kutoka Lyon, Julai 2017 na amekuwa akihusishwa na kurejea katika klabu yake hiyo ya zamani kwa uhamisho huru.

Lacazette alifunga mabao 71 katika mechi 206 akiwa na Arsenal na kushinda nao Kombe la FA mwaka 2020.

"Laca amekuwa mchezaji mzuri kwetu," alisema kocha wa Arsenal, Mikel Arteta wakati akizungumzia mustakabali wake.

"Amekuwa kiongozi wa kweli ndani na nje ya uwanja na amekuwa na ushawishi muhimu sana kwa wachezaji wetu wachanga.

"Ahadi yake kwetu imekuwa ya kipekee na tunamtakia yeye na familia yake mafanikio na furaha."

Lacazette alifunga mabao sita na kusajili pasi nane za mabao katika mechi 36 alizoichezea Arsenal msimu wa 2021-22.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# SINGIDA BIG STARS KUANZA KAMBI MAPEMA

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Singida Big Stars ambayo imepanda Ligi Kuu umesema timu yao inatarajiwa kuelekea mkoani Singida kwa ajili ya kuweka kambi ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi Kuu ya Tanzania bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa habari wa Klabu hiyo, Hussein Masanza alisema baada ya kumaliza mashindano ya Championship wachezaji walipewa mapumziko ya muda mfupi ili waipe miili yao muda wa kupumzika.

"Tunatarajia kwenda Singida hivi karibuni kuanza maandalizi ya Ligi Kuu Tanzania bara kwa msimu ujao, hasa ikizingatiwa sisi ni wageni kwenye mashindano hayo hivyo tunahitaji muda wa kutosha wa maandalizi," alisema Masanza.

**Alisema mikakati yao ni kusajili wachezaji wenye viwango vya juu kutoka ndani na nje ya nchi ambao wataleta ushindani kwenye Klabu yao.**

Aliongeza kuwa uongozi unaendelea kufanyia kazi mapendekezo ya kocha wao ambayo yamebainisha aina ya wachezaji anaowahitaji kwa ajili ya kukiboresha zaidi kikosi hicho.

"Tunasubiri dirisha la usajili lifunguliwe tuanze usajili wetu na tutawatangazia majina ya nyota ambao tutawasajili na tutakao achana nao, kwani tunataka tuboreshe zaidi timu yetu," alisema.

Alisema wadau wa soka hapa nchini watarajie makubwa kutoka kwao na kudai ushindani walioonesha kwenye Championship ndio ambao watauendeleza kwenye Ligi Kuu.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbas (katikati) akifungua mafunzo ya tasnia ya Filamu kwa Wasanii Chipukizi (Upcoming Film Stars) yaliyoendeshwa na Ofisi ya Bodi ya Filamu Tanzania Kivukoni hivi karibuni jijini Dar es Salaam. **PICHA: DENNIS FUSSI**



# Bondia Kiduku ajigamba Chokoraa kumdunda Uliza

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa Tanzania, Twaha Kiduku anaendelea kumnoa bondia Khalid Chokoraa ambaye anajiandaa kupambana na mpinzani wake, Omari Uliza katika pambano la raundi 4 la uzito wa kilo 68 litakalopigwa Juni 25 mwaka huu, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kiduku alisema maandalizi kuelekea katika pambano hilo yanaendelea vizuri katika kambi yao ya mjini Morogoro na wanajipanga kushinda raundi ya kwanza tu.

"Mazoezi yanaendelea vizuri nina imani na bondia wangu kutokana na aina ya mazoezi ninayompa," alisema Kiduku.

Alisema mpinzani wake ajiandae, kwani Chokoraa yupo vizuri ndio maana akaamua kwenda kuweka kambi mkoani humo.

Alisema lengo la bondia huyo kumfuata Morogoro ni kutokana na ubora aliokuwa nao hivyo ana nafasi ya kumpa ujuzi wake wote.

Kwa upande wa Meja Selemani Semunyu ambaye ni muandaaji wa pambano hilo alisema maandalizi yanaendelea vizuri na kwamba tiketi tayari zimeanza kuuzwa.

Aliomba wadau mbalimbali wa mchezo huo wajitokeze kwa wingi siku ya pambano kwani bila wao hakuna kinachowezekana.

"Ninaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi siku hiyo ya pambano hilo na hadi sasa tiketi zimeshaanza kuuzwa lengo ni kuzidi kuutangaza mchezo wa ngumi,"alisema Semunyu.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 05/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 3384 | OLS Oulu vs FC Vaajakoski | 1.67 | 4.05 | 3.95 |
| 14:00 | 4062 | Hittarps IK vs Onsala BK | 2.85 | 3.59 | 2.12 |
| 14:00 | 5282 | BK Forward vs Piteaa IF | 2.54 | 3.52 | 2.37 |
| 14:00 | 5782 | Orebro Syrianska vs Tegs SK | 1.23 | 5.68 | 8.81 |
| 15:00 | 2249 | IFK Kumla vs Ahlafors IF | 4.80 | 4.60 | 1.53 |
| 15:00 | 5937 | Korsnas IF FK vs Skiljebo SK | 5.92 | 4.83 | 1.38 |
| 16:00 | 1705 | Vietnam U23 vs South Korea U23 | 12.73 | 5.87 | 1.17 |
| 16:00 | 1849 | JJK Jyvaskyla vs GBK Kokkola | 1.12 | 7.67 | 12.79 |
| 16:00 | 3589 | Malawi vs Ethiopia | 2.25 | 3.03 | 3.38 |
| 16:00 | 4007 | San Marino vs Malta | 10.10 | 5.05 | 1.29 |
| 16:00 | 4061 | Stabaek W vs Avaldsnes W | 1.43 | 4.73 | 5.32 |
| 16:00 | 4150 | Pitea W vs Umea IK W | 1.61 | 4.04 | 4.34 |
| 16:00 | 4472 | Arna-Bjornar W vs Trondheims-Orn W | 13.00 | 8.20 | 1.13 |
| 16:00 | 5855 | Umeaa FC vs IF Sylvia | 2.26 | 3.33 | 2.79 |
| 17:00 | 1429 | Angelholms vs IK Oddevold | 2.55 | 3.33 | 2.45 |
| 17:00 | 1829 | Grimsby vs Solihull Moors | 3.04 | 3.39 | 2.17 |
| 17:00 | 2093 | Kiffen vs Jippo | 2.80 | 3.78 | 2.09 |
| 17:00 | 2492 | FC Trollhattan vs IFK Malmo | 1.50 | 4.32 | 4.91 |
| 17:00 | 2771 | Sandviken W vs Valerenga W | 2.21 | 3.75 | 2.75 |
| 17:00 | 3196 | Hogsby IK vs Rappe Goif | 4.03 | 3.84 | 1.69 |
| 17:00 | 3969 | Osterlen FF vs Kristianstads FF | 1.95 | 3.54 | 3.29 |
| 17:00 | 5208 | Raagsveds IF vs FC Jarfalla | 1.69 | 4.12 | 3.78 |
| 17:00 | 5823 | Belgium U21 vs Scotland U21 | 1.35 | 4.62 | 7.08 |
| 17:00 | 5908 | Juventude RS vs Fluminense | 2.76 | 2.95 | 2.51 |
| 18:30 | 1174 | FC Jazz vs HJS Akatemia | 1.58 | 4.32 | 4.23 |
| 18:30 | 1408 | FC Lapa vs Atlantis FC | 14.67 | 8.41 | 1.10 |
| 18:30 | 2041 | JS Hercules vs JBK Pietarsaari | 1.69 | 3.93 | 3.93 |
| 18:30 | 2083 | Peru vs New Zealand | 1.51 | 4.03 | 6.73 |
| 18:30 | 2418 | IF Gnistan vs Pepo Lappeenranta | 1.68 | 3.73 | 4.22 |
| 18:30 | 2581 | EIF Ekenas vs MP Mikkeli | 1.81 | 3.59 | 3.73 |
| 18:30 | 2712 | EPS vs Grankulla Ifk | 2.42 | 3.58 | 2.45 |
| 18:30 | 3851 | KuPS Akatemia vs FC Futura | 1.97 | 4.04 | 2.90 |
| 18:30 | 4289 | Nurmijarven Jalkapalloseura vs PPJ | 2.14 | 3.92 | 2.65 |
| 18:30 | 4476 | Ilves 2 vs Musa Pori | 2.70 | 4.10 | 2.17 |
| 19:00 | 1720 | Cyprus vs Northern Ireland | 3.47 | 3.27 | 2.10 |
| 19:00 | 2009 | Wales vs Ukraine | 2.65 | 3.01 | 2.85 |
| 19:00 | 3984 | Gibraltar vs North Macedonia | 17.21 | 6.88 | 1.15 |
| 19:30 | 3492 | Eibar vs Girona | 2.45 | 3.19 | 2.79 |
| 20:00 | 1681 | Colombia vs Saudi Arabia | 1.65 | 3.71 | 5.48 |
| 20:00 | 5029 | Costa Rica vs Martinique | 1.07 | 7.88 | 23.65 |
| 20:45 | 2663 | Ukraine U21 vs Macedonia U21 | 1.42 | 4.40 | 6.80 |
| 21:45 | 1025 | Sweden vs Norway | 2.05 | 3.27 | 3.62 |
| 21:45 | 2290 | Portugal vs Switzerland | 1.72 | 3.58 | 4.74 |
| 21:45 | 2329 | Serbia vs Slovenia | 1.46 | 4.12 | 7.04 |
| 21:45 | 3853 | Czech Republic vs Spain | 4.35 | 3.59 | 1.78 |
| 21:45 | 4996 | Bulgaria vs Georgia | 2.21 | 3.18 | 3.29 |
| 21:45 | 5650 | Kosovo vs Greece | 3.12 | 3.17 | 2.30 |
| 22:00 | 3661 | Egypt vs Guinea | 1.55 | 3.58 | 6.85 |
| 22:00 | 5220 | Palmeiras vs Atletico Mineiro | 2.24 | 3.14 | 2.99 |
| 22:00 | 5920 | Flamengo vs Fortaleza CE | 1.44 | 4.03 | 6.29 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Juni 5, 2022

Nipashe



Mane: Nitalazimika kuondoka Liver UKURASA 21



Mshambuliaji wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania, Twiga Stars, Opa Clement (kulia) akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Ethiopia wakati wa mchezo baina ya timu hizo jana kwenye mashindano ya CECAFA ya Wanawake yanayoendelea nchini Uganda. Timu hizo zilifungana 2-2. **PICHA: TFF**

## Try Again: Tutasajili kikosi tishio Afrika

**Na Adam Fungamwango**

MWENYEKITI wa Bodi ya Wakurugenzi wa Klabu ya Simba, Salim Abdallah 'Try Again', amesema wamejipanga kikamilifu kuirudisha timu kwenye ubora zaidi ya ule wa miaka miwili au mitatu iliyopita kwa kufanya usajili mkubwa ambao si tu utaifanya kuwa tishio nchini, bali Afrika nzima.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi, mwenyekiti huyo ameongeza kuwa ameongea na Rais wa Heshima wa Klabu hiyo na mwekezaji, Mohamed Dewji 'Mo', na kumhakikishia kuwa yupo tayari kufanikisha jambo hilo.

Wanachama na mashabiki wa klabu hiyo hivi wamekuwa wanyonge, hasa baada ya kuonekana kuukosa ubingwa msimu huu, kufungwa na Yanga bao 1-0 kwenye mechi ya nusu fainali ya Kombe la FA na kuondolewa kwenye michuano hiyo, huku pia wakishuhudia Kocha Mkuu, Pablo Franco akiondoshwa kwenye nafasi yake.

Pia msimu huu wameonekana kutoridhishwa na timu yao na wachezaji wao wengi kwa ujumla.

"Wanasimba wala msiwe na hofu, tumejipanga vilivyo kurudi kwenye ubora wetu. Tutarudi kwa kasi ya radi kwa jinsi tunavyofanya. Tutafanya usajili mkubwa ambao utatuwezesha kufanya vizuri kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika na Rais wa Heshima, Mohamed Dewji 'Mo' ameniambia yupo tayari kutoa pesa kufanikisha jambo hilo," alisema Try Again.

Alisema kufanikisha hilo ni lazima kwanza yafanyike maboresho makubwa kwenye kikosi na wao kama viongozi wameshajipanga kuanza zoezi hilo.

"Maboresho yanakuja kwenye kikosi na viongozi tumejipanga kufanikisha hilo. Tutasajili wachezaji ambao wana njaa ya mafanikio, tutabaki na wachezaji kadhaa, kuna wengine mikataba yao inaisha, wengine kutokana na viwango vya sasa kuwa chini tutawaaga, lakini pamoja na hayo nawapongeza sana wachezaji wetu, wamepambana kweli kweli," alisema.

Kuhusu kocha mpya atakayeinoa timu hiyo, Try Again alisema wapo kwenye mchakato kwani wametumiwa wasifu na makocha wengi, tunaendelea kuchuja ili kumpata atakayeendana na matarajio yetu na siku chache zijazo atakuwa amepatikana. Atakuja mapema ili ashiriki usajili pamoja na maandalizi ya msimu mpya," alisema mwenyekiti huyo.

# YANGA WAMZUIA MAYELE

**Na Saada Akida**

### ●●● Wakataa ofa kutoka RS Berkane iliyoletwa mezani kumsajili fowadi huyo, mwakilishi wa mchezaji...

DILI la Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele kwenda RS Berkane ya nchini Morocco linaonekana kuota mbawa baada ya viongozi wa klabu hiyo kuzuia mpango huo kwani wanamhitaji kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Hivi karibuni kulisambaa taarifa kwamba, uongozi wa Yanga wamepata ofa kutoka Klabu ya Berkane kuhitaji huduma ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Watu wa Congo (DRC).**

Taarifa za uhakika zilizofikia gazeti hili kutoka kwa mmoja wa vigogo wa Yanga ambaye hakutaka kutajwa jina lake gazetini, alisema walipata ofa kutoka Berkane ya kuhitaji huduma ya Mayele jambo ambalo uongozi umeikataa.

"Hatuwezi kumuuza mchezaji huyo kwa sababu bado yuko katika mipango yetu na ukizingatia huu ni muda wa usajili na tunatakiwa kuimarisha kikosi chetu kuelekea michuano ya kimataifa," alisema kiongozi huyo.

Aidha aliongeza: "Kwa sasa hatuwezi kumuuza mchezaji yeyote muhimu ndani ya kikosi cha timu, kwa sababu malengo yetu ni kufanya vizuri kwenye michuano ya Afrika."

Alisema Yanga haiwezi kuuza mchezaji ambaye yupo kwenye mipango yao, hivyo suala la Mayele kuondoka ndani ya klabu hiyo kwa sasa halipo, kwani bado wanahitaji huduma yake.

Nipashe lilimtafuta Mwakilishi wa Meneja wa mchezaji huyo, Nestory Mutuale ambaye alikiri kuwa ni kweli Mayele amepata ofa kutoka klabu ya RS Berkane, lakini viongozi wa Yanga hawatamuachia na sasa wako katika mchakato wa kumuongezea mkataba mwingine.

Alisema nyota huyo bado ana mkataba wa mwaka mmoja wa kuitumikia klabu hiyo na viongozi wa klabu yake sasa hawafikirii kumtoa Mayele, kwa sababu yuko katika mipango ya benchi la ufundi linaloongozwa na kocha Nabi (Nesredine) kwa ajili ya msimu ujao.

"Ni kweli hiyo ofa ipo na Berkane wanahitaji Yanga wakae mezani, lakini viongozi wake hawapo tayari kumtoa nyota huyo," alisema Mutuale.

9 770856 541002 >